# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO ARDHI NA NISHATI YA

## BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**FEBRUARI, 2024**

## YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA ........ 3
UTANGULIZI ........ 3
MUUNDO WA KAMATI ........ 4
MUDA WA KAZI ZA KAMATI ........ 5
NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA ........ 5
HADIDU REJEA ........ 6
SEHEMU YA PILI ........ 7
WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI ........ 7
UTANGULIZI ........ 30
WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI ........ 43
SEHEMU YA TATU ........ 67
HITIMISHO ........ 67

**RIPOTI YA KAMATI YA MAWASILIANO, ARDHI NA NISHATI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu cha 85 ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107 (1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, (Toleo la 2020).

Majukumu ya Kamati hii yameorodheshwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:

a) Kufatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
b) Kufatilia utekelezaji wa sera na mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Wizara ilizotoa katika Baraza;
c) Kufatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na miradi ya wananchi ya Wizara husika;
d) Kuchunguza na kufatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
e) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
f) Kushughulikia miswada ya sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
g) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
h) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati mbali ya majukumu yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Kanuni pia ina jukumu la kufatilia utekelezaji wa wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwemo Mashirika, Mamlaka na Vitengo vilivyomo ndani ya Wizara hizo. Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii ni: -

1. Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi
2. Wizara Ardhi na Maendeleo ya Makaazi
3. Wizara ya Maji, Nishati na Madini

**1:1 MUUNDO WA KAMATI**

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati imeundwa na Wajumbe wanane (8) na makatibu watatu (3) kama ifuatavyo:

| Nam | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Yahya Rashid Abdalla | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Aza Januari Joseph | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Ameir Abdallah Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohammed | Mjumbe |
| 9. | Ndg. Himid Haji Choko | Katibu |
| 10. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 11. | Ndg. Saad Othman Saad | Katibu |

### 1:2 MALENGO YA KAMATI

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kwa kufata malengo yafuatayo:

1. Kufatilia maagizo yaliyotolewa katika ripoti ya Kamati ya mwaka 2022/2023.
2. Kufatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa Mwaka 2023/2024.
3. Kufatilia utekelezaji wa Bajeti (kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo) kwa mwaka 2023/2024.
4. Kufatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara kwa Taasisi zake.

### 1:3 MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Katika mwaka wa fedha 2023/2024 Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ilifanya kazi zake kama ifuatavyo: -

1) Unguja kuanzia tarehe 14/08/2023 hadi tarehe 18/08/2023,
2) Pemba kuanzia tarehe 21/08/2023 hadi tarehe 25/08/2023,
3) Pemba kuanzia tarehe 06/11/2023 hadi tarehe 10/11/2023,
4) Unguja kuanzia tarehe 13/11/2023 hadi tarehe 17/11/2023,
5) Pemba kuanzia tarehe 15/01/2024 hadi tarehe 19/01/2024,
6) Unguja kuanzia tarehe 22/01/2024 hadi tarehe 26/01/2024.

### 1.4 NJIA NA MBINU ZILIZOTUMIKA

Katika kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa mujibu wa Kanuni, Kamati ilitumia njia na mbinu mbali mbali ikiwemo: -

*(i)* Kufanya vikao na Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara husika kwa lengo la kupata taarifa juu ya mambo au maswala mahsusi ambayo Kamati ilipenda kupata taarifa zake kutoka kwa watendaji wa taasisi hizo.

*(ii)* Kufanya ziara za ukaguzi katika miradi ya Maendeleo, sehemu za kazi na sehemu nyengine ambazo kwa namna moja ama nyengine zinahusika na utekelezaji wa majukumu ya Wizara husika.

*(iii)* Kufanya mikutano na Wafanyakazi pamoja na Wadau kwa lengo la kupokea maoni juu ya masuala mbali mbali ambayo Kamati ilikuwa inayafanyia kazi.

Kamati imebaini kwamba njia hizi ilizozitumia zimeleta manufaa makubwa, kutokana na njia hizo zimeweza kufahamu mafanikio na changamoto zinazoikabili Wizara na Idara husika katika utekelezaji wa majukumu yao.

## 1.5 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2023/2024 Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo; -

a) Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984.
b) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.
c) Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2020.
d) Hansard za Baraza za Mwaka 2023/2024.
e) Hotuba za Bajeti za Wizara zinazosimamiwa na Kamati hii.

## SEHEMU YA PILI

## WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### 2.0 MUUNDO WA WIZARA.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa sasa inaundwa na Idara tatu (3), Afisi kuu Pemba, Taasisi tisa (9) zinazojitegemea na Bodi mbili zinazosimamia sekta ya Ujenzi. Idara hizo ni; Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Mawasiliano na Afisi Kuu Pemba.

Taasisi tisa (9) zinazojitegemea ni pamoja na; Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Mamlaka ya Usafiri Baharini, Shirika la Bandari Zanzibar, Shirika la Meli Zanzibar, Wakala wa Barabara Zanzibar, Wakala wa Serikali wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar, Shirika la Mawasiliano (ZICTIA) na Wakala wa Majengo Zanzibar. Bodi zinazosimamiwa na Wizara hii ni Bodi ya Usajili Wakandarasi na Bodi ya Usajili wa Wataalamu, Wasanifu na Wakadiriaji Majengo.

### 2.1 IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Miongoni mwa majukumu makubwa ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kusimamia na kuratibu miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kamati imebaini kwamba kwa kipindi cha Julai – Disemba,2023 wizara kupitia Idara hii, imefanikiwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali inayohusu Ujenzi wa Barabara, Viwanja vya Ndege na Bandari ambayo ilipitishwa katika bajeti ya mwaka wa fedha, 2023/ 2024. Baadhi ya Miradi hiyo ni kama ifuatayo: -

#### 2:1:1 Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Mjini Unguja kilomita 100.9

Mradi huu unajumuisha ujenzi wa barabara za Mjini Unguja zenye urefu wa km **100.9** kwa kiwango cha lami. Aidha, unajumuisha ujenzi wa barabara za juu (Fly Over) katika eneo la Amani hadi Mwanakwerekwe “round about” ili kupunguza msongamano wa watumiaji wa barabara na vyombo vya usafiri katika maeneo hayo.

Kamati ilikagua kwa kufanya ziara na kupokea ripoti ya maendeleo ya mradi huu na imebaini kwamba hadi kufikia Disemba 31, 2023 utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 28.1% ikijumuisha shughuli zifuatazo: -

a) Kazi ya ujenzi wa Mitaro ya kupitishia maji kwenye kingo za Barabara pamoja njia za kupitishia miundombinu ya mawasiliano na maji kwa barabara ya Abeid Amani Karume Airport – Kiinua Miguu – Magereza km 6.5 imefanyika. Utekelezaji wa Barabara hii umefikia asilimia 99 %.
b) Mombasa Panned Area km 6.20 kazi zinaendelea kwa hatua mbali mbali ikiwemo uwekaji wa fusi kwa asilimia 79%.
c) Kwa barabara ya K/Samaki Junction Amani - Mtoni Junction Mkapa Road km 8.5, kazi ya uwekaji lami km 7 na uwekaji wa tabaka mbali mbali za kifusi kwa upande wa pili wa barabara zinaendelea na kufanya utekelezaji kufikia asilimia 46.66%.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaendelea kuishauri wizara kuongeza kasi ya ufuatiliaji na usimamizi wa mradi huu ili kuhakikisha Mkandarasi anafanya kazi kwa utaratibu na kasi inayohitajika na hatimae kukabidhi mradi kwa muda uliopangwa ili kupunguza kadhia kubwa ya msongomano wa magari katika maeneo ya mjini.

## 2:2 Mradi wa Ujenzi wa Barabara za ndani zenye Unguja na Pemba

Kamati iliarifiwa kwamba, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kazi za Ujenzi zinatekelezwa na Kampuni ya ARIS/ASER ya Uturuki na unasimamiwa na Wakala wa Barabara Zanzibar. Kamati imeshuhudia shughuli mbali mbali za utekelezaji wa mradi huu zikiendelea Unguja na Pemba ikiwemo usanifu, usafishaji na uwekaji wa kifusi na lami pamoja na ulipaji wa fidia za nyumba na vipando vilivyoathirika na ujenzi huo.

**2: 2:1 Ziara ya Kamati katika Ujenzi wa Barabara za ndani Pemba**

Kamati ilikagua maendeleo ya mradi wa Ujenzi wa Barabara za ndani kwa upande wa Pemba na kushuhudia shughuli za usafi kwa barabara zote za mradi huo Pemba, kuanza ujenzi kwa barabara ya Micheweni- Kiuyu-Mbuyuni Maziwangombe yenye urefu wa Kilomita 7.5 pamoja na barabara ya Mapofu- Tumbe Kojifa-Bandarini yenye urefu wa Kilomita 12.7 ambapo hadi tunatayarisha ripoti hii ujenzi unaendelea vizuri ingawa Kamati ilibaini baadhi ya changamoto kama ifuatavyo: -

**Changamoto za Ujenzi wa Barabara za Ndani Pemba**

a) Kuna kila dalili za kutuwama kwa maji baada ya Ujenzi huo.
b) Nyumba nyingi katika maeneo ya mradi zimejengwa kwa udongo, hivyo kuna hofu ya kuanguka endapo maji yanayotuwama hayatofanyiwa mpango wa kuhamishwa.
c) Kishindo cha Magari makubwa na zana za kazi kinaweza kuleta athari na uharibifu wa nyumba ambazo zipo karibu mno na barabara katika maeneo ya mradi.
d) Hakuna njia za kupitia maji ya mvua.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara ihakikishe inafanya tathmini ya awali na yenye kujitosheleza kabla ya kuteua maeneo ya miradi ya barabara za ndani ili kubaini athari zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.
2) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha inaweka Washauri Elekezi ambao ni Wazawa ili kuhakikisha mradi unapata ushauri sahihi na unaotekelezeka kulingana na jiografia na mazingira ya maeneo pamoja na maumbile ya udongo katika sehemu za Mradi husika.
3) Wizara iendelee kuhakikisha inakuwa na mashirikiano ya kisekta ili kila taasisi kuwa na njia za kupitisha miundombinu yake mapema na kuepusha uharibifu kwa kukata barabara muda mfupi tu baada ya ujenzi kukamilika.
4) Wizara ihakikishe inakuwa karibu na viongozi wa majimbo pamoja na Serikali za Mitaa ili ipate mashirikiano ya karibu wakati wa kutekeleza miradi hii ambayo moja kwa moja inawagusa wananchi hasa vijijini.

### 2:3 Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu Nne Unguja na Pemba.

Mradi huu unajumuisha Barabara ya Tunguu - Makunduchi kilomita 48.5, Fumba – Kisauni kilomita 12, Chake – Mkoani kilomita 43.5 na Barabara ya Wete – Chake kilomita 22.1.

**Utekelezaji wa miradi hii ni kama ifuatavyo: -**

Kamati ilifuatilia taarifa za mendeleo ya Utekelezaji wa Barabara ya Tunguu- Makunduchi, Fumba –Kisauni, na Mkoani- Chake Chake na kubaini kwamba hadi kufikia Disemba 31, 2023 hatua iliyofanyika ni kukamilisha kwa masharti ya mkataba wa mkopo ili kuweza kuomba fedha za awali (Advance payment) kwa ajili ya maandalizi ya kuanza mradi ambapo fedha hizo tayari zimepatikana. Kamati iliarifiwa kwamba kazi za ujenzi wa barabara hii zinategemewa kuanza ndani ya kipindi cha Robo ya tatu.

### 2:2:4 Ujenzi wa Barabara ya Chake- Wete

Kutokana na sababu mbali mbali za kimkakati, shauku na hamu, Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kwa makusudi imejipanga kila inapokuwa kisiwani Pemba kukagua Mradi mkongwe wa Barabara ya Chake –Wete ili kuangaliwa hatua inayofikiwa ya mradi huo.

Hadi kufikia Disemba 31, 2023, hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni uwekaji wa tabaka la kifusi kwa kilomita 13.5 kuanzia meli tano hadi Mzambarau takao kwa matabaka tofauti pamoja na kufanya matayarisho ya kutengeneza kitanda cha barabara (Road Bed) kwa urefu wa Kilomita 2 kuanzia Mzambarautakao hadi Machengwe, sambamba na ujenzi wa madaraja 2 (Daraja la Piki ambalo ujenzi wake umemalizika na Daraja la Machengwe ujenzi wake unaoendelea).

Aidha, Kamati imeshuhudia matayarisho kwa ajili ya kuweka fusi tabaka la mwisho pamoja na maandalizi ya uwekaji wa lami yakiendelea kwa kilomita 6 za mwanzo. Kwa ujumla takwimu za ujenzi wa Barabara hii zinaonesha kwamba umefikia asilimia 30%.

Kwa upande wa malipo ya fidia za nyumba pamoja na vipando vya wananchi waliotakiwa kuondoka kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Barabara hiyo tayari umekamilika kuanzia Melitano hadi Limbani ambapo jumla ya wananchi wapatao 607 wamefanyiwa malipo.

**Changamoto Katika Ujenzi wa Barabara ya Chake- Wete**

a) Kamati imebaini kuna Wananchi 7 bado hawajafanyiwa malipo ambapo ucheleweshaji wa malipo hayo ulitokana na baadhi ya wananchi hao kufanyiwa tena mapitio ya tathmini zao baada ya kuonesha kuto kuridhika.
b) Ucheleweshaji wa upatikanaji wa taarifa na thamani kwa sehemu za baraza, vibanda vya biashara na baadhi ya nyumba ambazo zinatarajiwa kuathirika wakati wa ujenzi hususan katika maeneo ya Limbani hadi Kilimandege.
c) Mjenzi wa Barabara hiyo kubadilisha msimamizi wa ujenzi (Project Manager) kila mara.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara ihakikishe inashirikiana na taasisi zote zinazohusika na masuala ya fidia ili mkandarasi aendelee na shughuli zake bila ya vikwazo vyovyote.
2) Kufuatia kasi ndogo ya ujenzi na visingizio vya kila siku na sababu za kila aina kwa mkandarasi wa barabara hii, Kamati inaiomba serikali kufanya tathmini ya kina kuhusiana na uwezo wa Mkandarasi huyo ikiwa ni njia moja wapo ya kuhimiza ujenzi huo.
3) Kamati inashauri sehemu ndogo inayokwisha kukamilika kwa kifusi iwekwe lami kama vile inavyoonekana katika barabara ya Kiembe Samaki – Amani ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kwa kifusi hicho kukaaa muda mrefu na barabara kuanza kuchimbika kabla ya ujenzi wa lamu kuanza.

### 2:2:4 Mradi wa Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba

Kamati pia ilifuatilia Mradi wa Uimarishaji wa uwanja wa ndege wa Pemba ili ukidhi mahitaji ya ongezeko la abiria na wakati wa sasa. Kamati imebaini kwamba mradi huu nao umefikia hatua ya kukamilishwa kwa masharti ya mkataba wa mkopo ili kuweza kuomba fedha za awali (Advance payment) kwa ajili ya maandalizi na kuanza mradi. Kazi za ujenzi wa mradi huu zinategemewa kuanza ndani ya kipindi cha robo ya tatu.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati Wizara Kabla ya kuanza Utekelezaji wa Mradi Uimarishaji wa Uwanja wa Ndege wa Pemba kuhakikikisha wananchi wote wamelipwa stahili ya fidia kulingana na thamani na muda iliopo.

### 2:2:4 Ujenzi wa Bandari Jumuishi ya Mangapwani (Ujenzi wa Barabara za Ndani ya Eneo la Bandari ya Mangapwani (Ring Road) km 12)

Hadi kamati imepokea taarifa hii kazi ya ujenzi inaendelea na imefikia asilimia 30 ambayo kwa upande wa Barabara ya magharibi yenye kilomita 4.4 kazi zilizokamilika ni kuweka tabaka la msingi (sub-base) kufikia kilomita 4.25, Ujenzi wa kalvati (culverts) saba (7), ujenzi wa misingi ya kupitisha maji ya mvua (Concrete Channel) unaendelea kujengwa kwa kiasi cha mita 2500. Aidha, kwa upande wa njia ya kaskazini yenye kilomita 1.2, kiasi cha mita 950 zinaendelea kujazwa kifusi kwa tabaka la chini (15 bottom - Subgrade).

Aidha, kamati imebaini kwamba kazi ya tathmini ya fidia ya Barabara ya Mashariki na Kusini ambayo imehusisha maeneo ya Mangapwani, Kidanzini na Makoba inaendelea kufanyiwa tathimini ya nyumba na vipando kwa maeneo yaliyoathirika na Barabara na kufikia asilimia 80%.

## 2:3 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI.

Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani miongoni mwa majukumu yake ni kusimamia usalama kwa watumiaji wa barabara Unguja na Pemba pamoja na kusimamia shughuli za Kamati ya Usalama Barabarani ambayo imepewa jukumu la kupunguza ajali zinazosababisha vifo, majeruhi na ulemavu wa kudumu.

### 2:3:1 Ajali za Barabarani

Kamati ilikutana na watendaji wa Mamlaka ya usafiri na Usalama Barabarani na kubaini kwamba katika kipindi cha Julai - Disemba, 2023, jumla ya ajali za barabarani **100** zimeripotiwa kutokea Unguja na Pemba, kati ya ajali hizo, vifo ni **103** na majeruhi **116**.

### 2:3:2 Adhabu za Papo kwa Papo

Katika kudhibiti suala zima la kupunguza ajali na makosa ya barabarani, Mamlaka ya Usafiri na Usalama barabarani ilitengeneza Kanuni za Adhabu za papo kwa papo na zimeanza kutumika tangu mwezi Aprili, 2023. Kamati imebaini kuwa katika kipindi cha Julai – Disemba 2023, jumla ya makosa 14,806 yenye thamani ya TZS 323,716,500 yameripotiwa, kati ya makosa hayo makosa **9,331** yamelipiwa sawa TZS **215,723,900** na makosa **5,475** ni madeni sawa na TZS **107,992,600.**

**Changamoto za Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani.**

Kamati imebaini kuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Usafiri wa Barabarani, Mamlaka hii inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazopunguza ufanisi wa utendaji ikiwemo mfumo wa adhabu za papo kwa papo. Changamoto hizo ni hizi zifuatazo;-

a) Kumaliza muda kwa nambari ya malipo (Control number) ya adhabu za papo kwa papo kunakosababishwa na kucheleweshwa kwa malipo kwa muda uliowekwa na kushindwa kutumika kwa nambari ya malipo iliyoisha muda.

b) Wananchi kuchelewa kufanya malipo ya adhabu kwa wakati kunakopelekea kurundikana kwa madeni.

c) Kutokutumika ipasavyo mfumo pamoja na mashine za POS jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa makosa barabarani.

d) Mashine za POS kutumika kwa matumizi mengine kama vile kuweka game pamoja na azam tv katika vifaa hivyo.

e) Uhaba wa vyuo vya udereva hasa Vijijini.

f) Nidhamu ndogo kwa madereva wa Boda boda.

g) Changamoto ya kupakia kupita kiasi kwa gari zinazochukua wanafunzi (School Bus).

h) Wafanyakazi wa Mamlaka pamoja na uwezo wa Taasisi yao wa kugharamia ulipaji wa mishahara na uendeshaji, unyeti wa huduma wanazotoa pamoja na Mchango wa Taasisi yao katika Mfuko Mkuu wa Hazina, bado hawajabadilishiwa mafao ya stahiki zao (Mishahara) kutoka iliyokuwa Wakala na kuwa Mamlaka.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Wizara kupitia Mamlaka ifanye marekebisho juu ya namna bora ya utekelezaji wa mfumo wa adhabu za papo kwa papo ili changamoto zilizojitokeza ikiwemo kumaliza muda kwa nambari ya malipo ziweze kurekebishwa.
2. Kamati inaishauri Mamlaka na Wizara kwa ujumla kusimamia suala la uanzishwaji wa vyuo vya Udereva hadi vijini ikiwa ni njia moja wapo ya kuongeza uwelea kwa wananchi juu ya masuala ya usalama wa barabarani.
3. Mamlaka izidishe kasi ya Usimamizi wa Sheria na Miongozo ya Usalama barabarani ikiwemo waendesha bodaboda ili kupunguza ajali na vifo vinavyochangia kupunguza nguvu kazi ya taifa.
4. Wizara iweke utararibu na miongozo maalum kwa gari zinazochukua wanafunzi ili kupunguza tatizo la mrundikano na upakiaji mbaya wa wanafunzi katika gari hizo.
5. Wizara ifuatilia stahiki za Wafanyakazi wa Mamlaka kutoka Wakala na kuwa ya Mamlaka.

## 2:4 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

Katika kipindi cha Julai – Disemba, 2023, Shirika la Bandari limefanikiwa kutoa huduma za mizigo na meli ambapo jumla ya tani za mizigo mchanganyiko 245,595, makontena 14,528 pamoja na tani za mzigo wa majahazi 152,925 zimehudumiwa. Aidha, jumla ya meli za kigeni 26, meli za ndani 1,217 na majahazi 3,139 yamepatiwa huduma.

Aidha, katika kuimarisha miundombinu ya Bandari, Shirika la Bandari, linaendelea kusimamia na kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo kukamilisha matengenezo ya bandari ya Mkoani kwa asilimia 100, kuendelea na ujenzi wa Bandari ya Shumba ya Mjini, kukamilisha matengenezo ya Bandari ya Mkokotoni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu (Feasibility Study) ya Bandari ya Wete inayoonesha urefu na aina ya gati, kina cha maji pamoja na aina ya majengo kulingana na ardhi ya eneo hilo. Aidha, michoro ya Bandari hiyo imekamilika na inajumuisha mchoro wa gati, ghala la kuhifadhia mizigo na sehemu ya kupumzikia abiria pamoja na afisi za wadau.

### 2:4:1 Hali halisi ya Bandari ya Malindi Baada Kupewa Muekezaji

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi chini ya Taasisi yake ya Shirika la Bandari ilifunga mkataba tarehe 18 Mei, 2023 na Afrika Global Logistic (AGL) ambayo inayotoa huduma za kibandari nchi mbali mbali. Kampuni hiyo inategemea kuendesha Bandari ya Malindi kwa kipindi cha miaka mitano imesajiliwa kwa jina la Zanzibar Multipurpose Terminal (ZMT).

Kampuni ya ZMT inashughulika na utoaji wa huduma za meli za makontena pamoja na mizigo katika Bandari kuu ya Malindi ambapo kupitia makubaliano ya Mkataba, wafanyakazi 390 (wanaume 282 na wanawake 108) wanaotoka katika Idara mbali mbali za Shirika walihamishiwa katika Kampuni hiyo.

Utafiti wa Kamati umebaini kuwa kuanzia tarehe 18/09/2023, Kampuni ya ZMT ilikabidhiwa rasmi Bandari ya Malindi kwa ajili ya kuanza kutoa huduma ya uendeshaji wa bandari, ndani ya muda huo Serikali kupitia Shirika la Bandari na Wizara imekuwa ikifanya kazi kwa karibu na ZMT pamoja na wadau wa Bandari katika kusikiliza changamoto mbali mbali ambazo hujitokeza kutokana na mabadiliko ya uendeshaji katika Bandari hiyo.

### 2:4:2 Mafanikio ya Bandari ya Malindi baada kupewa Muekezaji

Kamati imepokea taarifa kutoka ndani ya Shirika la Bandari ambazo zinabainisha kuwa baada ya kupewa muekezaji katika Bandari ya Malindi, kumepatikana mafanikio yafuatayo;-

1. Wafanyakazi wa Shirika wamepatiwa mafunzo ya udereva kwa vitendo kutoka kwa Mtalaamu aliyetokea Afrika Kusini ili kuweza kufanyakazi kwa ufanisi;
2. Kuongezeka kwa Stahiki za wafanyakazi (incentives) pamoja na mishahara yao;
3. Ulinzi na usalama umeimarika ikiwemo kuingia na kutoka kwa watu na vyombo vinavyoingia bandarini;
4. Kutumia mifumo ya technologia ya kisasa katika kutoa huduma za kiforodha.

5. Kanuni za miongozo ya Bandari (International Safety Standard) inaendelea kufatwa vyema ambayo inasimamiwa na International Maritime Organization (IMO)

### 2:4:3 Changamoto za Bandari ya Malindi Baada Kupewa Muekezaji

Kamati ilifanya vikao tofauti na Viongozi wa Shirika la Bandari, wadau wa bandari pamoja na uongozi wa ZMT ambao walibainisha changamoto zilizojitokeza pamoja na jitihada zilizochukuliwa ili kuzitatua kama ifuatavyo; -

a) **Ufanisi Mdogo Katika Utoaji wa Huduma kwa Meli za Makasha "container".** licha ya kuengezeka ufanisi katika ushushaji wa makasha meli zimekuwa zinachukua muda mrefu kabla ya kufunga gatini na wakati wa kuondoka gatini: Baada ya kufatilia kwa karibu ZMT walikiri kuengezeka muda wa meli kukaa gatini, kwa takriban asilimia (75%) ya makasha yaliyopo katika maeneo ya kuhifadhia mizigo (Malindi, Bwawani na Maruhubi) ni makasha matupu (empty) hali hii imesababisha msongamano. Hata hivyo, Kamati iliarifiwa kwamba jitihada zimechukuliwa na tayari makasha haya yameondolewa na kupatikana nafasi zaidi ya kuhifadhia mizigo na kuwezesha Bandari kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

b) **Kuengezeka kwa Tozo za Bandari kwa Wadau wa Majahazi na Meli za Ndani na Utayari wa Kulipia Huduma za Bandari Kama Muongozo wa Tozo Unavyoelekeza.** Malalamiko haya yalipokewa kutoka kwa wadau ambapo Serikali imejibu kwamba hakuna mabadiliko ya tozo za huduma za Bandari kwa sasa. Kwa mujibu wa mkataba, kampuni ya ZMT imetakiwa kusimamia utoaji wote wa huduma unaolipiwa kupitia tozo rasmi (ZPC Tariff Book). Lengo kuu ni kuhakikisha huduma zote zinalipiwa kwa mujibu wa taratibu zinavyoongoza ili kuepusha uvujaji wa mapato ya Shirika.

c) **Kubadilika Utaratibu wa Malipo na Utoaji wa Huduma kwa Meli za Ndani (local vessel).** Kamati ilipokea malalamiko kutoka umoja wa wamiliki wa meli za Zanzibar (Zanzibar Ship Owners Association) juu ya mabadiliko ya kutolewa

huduma kwa meli zao na ikiwemo mabadiliko ya tozo kwa huduma kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini (Zanzibar Maritime Authority (ZMA)) ambae ni msimamizi wa leseni wa vyombo hivo. Hata hivyo, Kamati ilifuatilia kwa kina suala hili na kubaini kwamba baada ya kutolewa taaluma imeonekana hakuna malipo mapya isipokuwa utaratibu tu ulikuwa haujafahamika kwa wahusika wa meli za ndani.

d) **Kuchelewa Kutoka kwa Mizigo ya Wateja Baada ya Kukamilisha Hatua za Malipo.** Kamati ilimepokea malalamiko kutoka umoja wa wakala wa forodha (Zanzibar Freight and Forward Bureau – ZFB) juu ya uchelewaji wa kutoka kwa mizigo ambayo imekamilisha taratibu zake. Hata hivyo, Kamati iliarifiwa kwamba Wizara na uongozi wa ZMT imefanya vikao na wadau husika ikiwemo wafanyabiashara wakubwa wanaohusika na uletaji wa bidhaa nchini (big importers), uongozi wa wakala wa forodha (ZFB), kwa lengo la kuifahamu changamoto hii imesababishwa na namna ya kuitatua.

### 2:4:4 Bandari ya Mkoani

Katika kipindi hiki bandari ya Mkoani imefanyiwa maboresho makubwa ambako kazi mbali mbali zimefanyika kwa lengo la kuifanya Bandari hii kuweza kutoa huduma zilizo bora kwa Meli za kitaifa na kimataifa. Kamati ilikaguwa Mradi huu na kushuhudia kazi zilizofanyika katika mradi huu ni kama zifuatazo: -

i. Kujenga eneo la kuhifadhia makontena **(Container Yard)** yenye uwezo wa kuhifadhi makontena **580** kwa wakati mmoja.
ii. Kujenga ukuta wa kuzuia maji ya Bahari **(Retaining Wall)** wenye urefu wa mita **120.**
iii. Kujenga njia watembea kwa miguu **(Course way)** yenye upana wa mita mbili na nusu **(2.5)** upande wa Kaskazini juu ambayo imeezekwa vyema ili kuwakinga abiria na jua au mvua.
iv. Kutanua barabara kuu ya kupitishia magari ya mizigo pamoja na vyombo vyengine.

v. Ukarabati wa gati **(Jetty Slab Repairing)**, kwa lengo la kuondosha mipasuko, nondo zilizooza na kubadilisha viguzo vya kufungia meli katika gati, ili kuifanya iwe imara zaidi na kutumika kwa muda mrefu.

### 2:4:5 Sehemu za Ukaguzi wa Abiria na Mizigo Bandarini na Uwanja wa Ndege

Katika nyakati tofauti, Kamati imepokea malalamiko ya matumizi mabaya pamoja na kuvunjiwa heshima baadhi ya abiria hasa viongozi katika sehemu za upekuzi wa abiria na mizigo sehemu ya abiria wa kawaida pamoja na ile ya Watu mashuhuri (VIP) ndani ya Bandari ya Zanzibar, Bandari ya Mkoani, Uwanja wa Ndege Zanzibar pamoja na Uwanja wa Pemba.

### 2:4:6 Bandari ya Wesha

Kamati imebaini kwamba pamoja na kuwa miundo mbinu ya Bandari ya Wesha ni ya zamani, lakini bado Bandari hii inaendelea kutoa huduma mbali mbali kwa vyombo vya baharini ikiwemo Meli na Majahazi kutoka maeneo mbali mbali ya jirani na kisiwa cha Pemba.

**Changamoto za Bandari ya Wesha**

a) Kuchakaa kwa miundombinu ya bandari.
b) Vyombo kushindwa kufika gatini wakati maji yanapotoka.
c) Uhaba wa Ofisi kwa taasisi nyengine zinazofanya kazi katika bandari hiyo.

### 2:4:7 Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini.

Mkataba wa kusanifu na kujengwa kwa Bandari ya Shumba Mjini ulisainiwa tarehe 27 Juni 2023, kati ya Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) na Kampuni ya Comfix & Engineering Smart Solution. Kukamilika kwa Bandari hiyo kutasaidia kuongeza huduma za usafiri na usafirishaji baharini baina ya kisiwa cha Pemba na maeneo jirani, kufungua milango ya shughuli za utalii baina ya Zanzibar na nchi jirani hasa Kenya pamoja na kuimarisha mahusiano zaidi kati ya watu wa Kenya na Zanzibar.

Kamati ilikagua maendeleo ya ujenzi huo, ingawa unakwenda kwa kasi ndogo kabisa, lakini Mkandarasi amekwisha zungusha uzio, kufanya utafiti wa maumbile ya ardhi katika eneo la ujenzi pamoja na uchimbaji, utafiti wa udongo na mwamba wa bahari ambapo ripoti ya kazi

hizo imeshawasilishwa kwa Shirika na kazi ya kusarifu na kuandaa michoro ya ujenzi huo nayo imekamilika. Hata hivyo Kamati imebaini kwamba kazi za Mradi huu ilisita kutokana na sababu mbali mbali za kiufundi na badala yake unapelekwa Kota inayofuata kwa ajili ya utekelezaji.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara ihakikishe inapokea na kufanyia kazi changamoto zote zinazotolewa na Wadau ili kuhakikisha Bandari ya Malindi inafanyakazi kwa ufanisi mkubwa ili kutimiza azma ya Serikali juu ya uendeshaji wa bandari hiyo.
2) Pia, Kamati inaendelea kushauri Wizara kuwa na utaratibu mzuri wa mafunzo kwa wafanyakazi wake hasa mafunzo ya Huduma kwa Wateja (**Customer Care**) kwa watendaji wanaotoa huduma moja kwa moja kwa wananchi.
3) Kuwekwa utaratibu maalum utakaozingatia matumizi sahihi ya eneo la watu mashuhuri (VIP) katika Bandari ya Zanzibar, Mkoani, Uwanja wa Ndege wa Zanzibar na Pemba.
4) Wizara ihakikishe inasimamia vizuri suala la Ujenzi wa Makaazi ya watu karibu na Bandari Kavu ya Fumba pamoja na Ulinzi na usalama wa eneo hilo.
5) Wizara ihakikishe inazifanyia kazi Changamoto za Bandari ya Wesha ikiwemo uchakavu wa miundombinu pamoja kuhakikikisha inatenga nafasi kwa ofisi zote za taasisi zinazofanya kazi bandarini hapo ili shughuli kibandari zifanyike kwa ufanisi zaidi.
6) Kamati inaomba Wizara kutoa maelezo juu ya kusua sua kwa ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini ambayo ni miongoni mwa Miradi ya Kimkakati na tegemeo kubwa la wananchi wa wilaya ya Micheweni.

## 2:5 WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

Katika kuhakikisha kuwa barabara za Unguja na Pemba zinapitika na kuwa safi , Wakala wa Barabara Zanzibar kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023 imefanikiwa kukamilisha matengenezo ya barabara mbalimbali kwa kiwango cha lami ikiwemo barabara ya Fuoni Ijitimai -Msikiti Al Rahman (0.6km), barabara ya Mtoni Kidatu – Garagara (3.0km),

Barabara ya kipapo-Mgelema (5.3km) pamoja na uwekaji wa kifusi na lami ya maji kwa barabara ya Magogoni- Hospital, Kitogani – Hospital, Hanyegwamchana, soko la wajasiriamali na Mama Samia Primary School. Aidha, kazi za matengenezo kwa barabara mbalimbali za Unguja na Pemba zilifanyika ikiwemo barabara ya Kinazini - Bububu, barabara ya Uwanja wa Amani na barabara ya Machomane – Wawi. Vilevile, kazi za ukataji majani, usafi wa madaraja na kalvati pamoja na uzibaji wa mashimo kwa Barabara mbalimbali za lami Unguja na Pemba zimefanyika.

**Changamoto za Wakala wa Barabara Zanzibar**

Baada ya kupokea ripoti mbali mbali za Wakala wa Barabara pamoja na kufanya ziara katika meneo mbali mbali ya utekelezaji wa Wakala, kamati imegundua changamoto zifuatazo;-

a) **Uchakavu na Uwepo wa Mashimo Katika Njia Nyingi Unguja na Pemba:** Barabara (njia) nyingi za ndani zinaharibika kila mara hasa kipindi cha mvua jambo linalopekea ugumu katika harakati za usafiri katika maeneo ya mjini na vijijini kama vile barabara ya ndani kutoka Kwaboko – Kidongo Chekundu - Meya.
b) **Uhaba Mkubwa wa Vifaa vya Ujenzi wa Barabara:** Wakala inakabiliwa na uhaba mkubwa wa vifaa vya ujenzi ukilinganisha na kazi zilizopo Unguja na Pemba. Kamati imeshuhudia vifaa vingi ikiwemo magari ni vya muda mrefu, na vyengine vimeuzwa vikiwa mali chakavu. Hali hii, inapelekea Wakala kushindwa kutimiza majukumu yake kama inavyotakiwa.
c) **Uhaba wa Wafanyakazi:** Wakala ina upungufu mkubwa wa wafanyakazi hasa kwenye kada za wataalamu wakiwemo mafundi wa zana na mitambo.
d) **Uhaba wa Fedha za Uendeshaji wa Ofisi na Utekelezaji wa Miradi:**
e) **Uvamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Barabara kwa Ujenzi Holela:** Kamati imebaini kwamba changamoto hii inatokana na usimamizi mdogo wa sheria zilizopo kwa taasisi mbali mbali zinazohusika na masuala ya ujenzi.
f) **Wizi na Uharibifu wa Alama za Barabarani:** Changamoto hii imekua ya muda mrefu sana na inaendelea kujitokeza kutokana na madai ya ugumu wa usimamizi wa

suala hili na kutokuwepo mashirikiano baina ya Serikali za mitaa na vyombo vya Ulinzi na Usalama katika kuchukua hatua kwa wanaobainika kufanya kosa hili.

g) **Uhaba na Uchakavu wa Majengo ya Ofisi, Maabara na Karakana**: Kamati imejuilishwa kwamba Wakala wa barabara ina changamoto ya muda mrefu sana ya uhaba na uchakavu wa majengo ya ofisi, maabara na karakana.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.**

1) Kamati inaiomba Wizara kupitia Wakala wa Barabara ifanye jitihada za kutafuta suluhisho la kudumu la kudhibiti kuchimbika ovyo kwa barabara zetu na kuondosha adha ya barabarani hasa wakati wa mvua.
2) Wizara ifanye jitihada ya kuomba Serikalini fedha za makusanyo zinazokusanywa na Wizara ya fedha zinazopelekwa mfuko wa Barabara kwa ajili ya matengenezo ya barabara ziingizwe na kutumika kama malengo ya fedha hizo yalivyokusudiwa.
3) Wizara ifanye mazungumzo na taasisi mbali mbali ili kuweza kusaidiana katika kusimamia utekelezaji wa sheria zilizopo na kuweza kudhibiti changamoto ya uvamizi wa hifadhi ya barabara kwa shughuli za ujenzi na biashara.
4) Wizara iendelee kuchukua hatua za kutoa taaluma kwa jamii juu ya umuhimu wa uwepo na matumizi ya alama za barabarani na hasara inayopatikana kwa jamii na Serikali iwapo vitendo vya wizi na uharibifu wa alama hizo vikiendelea.

## 2:6 WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

Wizara imeiripotia kamati kwamba kupitia taasisi yake ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar katika kipindi cha Julai – Disemba, 2023 imefanikiwa kuzifanyia matengenezo gari za Serikali na binafsi 822 kwa Unguja na Pemba. Kati ya gari hizo, gari 746 ni za Serikali na gari 76 ni za watu binafsi. Aidha, Wakala wa Karakana kuu ya Serikali ilikadiriwa kukusanya Tsh 49,000,000 sawa na asilimia 100 ya utekelezaji.

Katika hatua nyengine Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, inadai **jumla ya TZS 60,684,025** kwa taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zimepata huduma katika karakana kuu kwa kipindi hicho.

**Changamoto za Wakala wa Karakana Kuu ya Magari**

Wakala wa Karakana Kuu ya Magari katika kutekeleza majukumu na shughuli zake, bado inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Uhaba wa bajeti na fedha za matumizi ya kawaida inayopelekea Karakana na vitengo vyake kushindwa kutekeleza shughuli zake kama ilivyojipangia pamoja na kupelekea upungufu wa vipuri na vilainishi kwa ajili ya Karakana.
b) Uhaba wa vitendea kazi katika karakana zote kwa ajili ya mafundi na Maafisa ikiwemo, jeki, stand, compyuta na vitu vya samani.
c) Kutokea kwa matengenezo yasiyotarajiwa (upana wa dhana ya ufundi) pamoja na kuwepo kwa vipengele vya sheria za manunuzi vinavyopelekea kuchelewa kupatikana kwa vifaa na vipuri vinavyohitajika kwa uharaka.
d) Elimu ndogo kwa mafundi pamoja na uhaba wa mafundi katika vitengo husika na kukosekana kwa wataalamu wabobezi wa ufundi wa magari ya kisasa.
e) Uchakavu pamoja na kupitwa na wakati kwa miundombinu ya Karakana, mashine na vifaa kwa ajili ya huduma za kisasa za kiufundi.
f) Kukosekana kwa majengo maalumu ya Ofisi za kiutawala na kutumia majengo ambayo yanashuhulika na shughuli za ufundi wa magari kama ofisi jambo ambalo linahatarisha afya za maafisa na usalama wa nyaraka za Serikali.
g) Kuchelewa kulipa madeni kwa baadhi ya Taasisi za Serikali baada ya kupatiwa huduma na kupelekea Karakana kukusanya mapato madogo yasiyoridhisha.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI.**

1) Kamati inaishauri Karakana kuomba kuruhusiwa kutumia mapato yatokanayo na matengenezo ya magari.
2) Wakala iendelee kufuatilia upajikanaji wa ruhusa ya kufanya matumizi ya dharura na ya haraka bila kutumia mfumo wa Manunuzi.
3) Wakala iweke utaratibu mpya wa malipo kwa wateja wote wanaopatiwa huduma ya matengenezo ambapo mteja atakiwe kulipa kwanza kabla ya kufanyiwa matengenezo ya gari yake.

## 2:7 SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati pia ilitafuta taarifa za Shirika la Meli Zanzibar ambapo imebaini kwamba kwa kipindi cha Julai – Septemba, 2023, Shirika limefanikiwa kufanya safari 19 za meli ya MT Ukombozi II za kusafirisha nishati ya mafuta kutoka bandari ya Tanga na kupeleka katika Bandari ya Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya Meli 198 za kigeni zimepatiwa huduma ya uwakala katika kipindi hicho. Kwa upande wa Meli ya MV Mapinduzi II, matengenezo ya meli hiyo yanaendelea na yameshafikia asilimia 80.

### Changamoto za Shirika la Meli Zanzibar

Kamati imebaini kuwa katika kuendesha shughuli zake, Shirika limekuwa likikabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo; -

a) Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma katika shughuli za kibiashara za Shirika.

b) Kutokuwepo na mfumo wa mishahara ya ubaharia na kutotambulika katika taasisi za kiutumishi za Serikali.

c) Shirika kutegemea Meli moja tu ya MT Ukombozi II ambayo kwa sasa imekodishwa kwa Kampuni ya GBP Tanzania Limited kwa kodi ya safari (Voyage charter).

### MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

1) Kamati inaishauri Serikali kuwa ipo haja ya kununua meli nyengine mpya yenye ubora inayolingana kimatumizi na MT Mkombozi II.
2) Vile vile, Kamati inaisisitiza Serikali inapofanya manunuzi ya vyombo vya usafiri itizame zaidi mahitaji halisi ya wakati uliopo na ujao ikiwa ni pamoja na kutafuta vyombo ambayo vitakuwa na unafuu wa kuuzika au kuingia ubiya pale itakapohitajika.
3) Kamati inaishauri wizara na Serikali kwa ujumla kuliruhusu Shirika kununua vifaa au vipuri moja kwa moja kutoka kwa wasambazaji hata kama mara nyingi

wasambazaji hao huwa kutoka nje ya nchi ambao hawamo katika mfumo wa manunuzi Serikalini.

4) Kamati inaomba Serikali kupitia wizara ya Utumishi iweke mfumo wa mishahara ya mabaharia kama inavyohitajika kulingana na kada hiyo.

5) Kamati inaendelea kusisitiza juu ya ukamilishwaji wa matendengenezo ya MV Mapinduzi 11 kwani shughuli hiyo imekuwa ni ya muda mrefu na kukatisha tamaa kwa wananchi hasa wale wa kipato cha chini wanaotegemea usafiri wa Majini .

## 2:8 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI (ZMA)

Katika kuhakikisha kuwa usalama wa safari za baharini kitaifa na kimataifa unakuwepo muda wote, Wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023 imefanikiwa kusajili meli 169 katika usajili wa kimataifa na kuingiza jumla ya TZS 1,878,064,000 ikiwa ni mapato ya usajili huo na kwa usajili wa ndani ZMA imefanikiwa kusajili meli 9 katika kipindi hicho. Aidha, kazi ya ukaguzi wa meli uliendelea ambapo jumla ya meli za ndani 30 na meli za nje 256 zilikaguliwa, ukaguzi wa meli za nje hufanywa na wakaguzi wa kimataifa (RO'S) kwa niaba ya ZMA. Aidha, katika kusimamia usalama wa abiria, ZMA imefanikiwa kuwahudumia abiria 917,344 na kusimamia safari za meli 2,377 Unguja na Pemba.

### 2:8:1 Kuimarika kwa Sekta ya Usafiri wa Majini Zanzibar

Katika kukagua kuimarika kwa Usafiri wa majini, kamati ilisafiri na Boti ya *Zanzibar 3,* inayomilikiwa na kampuni ya Zanzibar First Ferries inayofanya safari zake kutoka Unguja/Pemba na Tanga. Kamati imeshuhudia uimara wa boti hiyo inayokwenda kwa kasi ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza changamoto ya usafiri kwa wananchi wa Unguja, Pemba na Tanga.

### Changamoto za Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA)

Kamati ilifanya mahojiano ya ana kwa ana na watendaji wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar kuhusiana na mafanikio na changamoto zinazowakabili katika utendaji wao na walibainisha yafuatayo; -

a) **Mamlaka kutopatiwa CALL SIGN kutoka TCRA:** Kwa muda mrefu Mamlaka imekuwa ikiomba Call Sign kutoka TCRA ambapo pamoja na kukutana na kufanya vikao na wahusika wa TCRA, bado TCRA inachelewa kutoa huduma hiyo kwa wakati na kusababisha uzoroteshaji wa usajili wa meli za kimataifa ambao una ushindani mkubwa.

b) **Mamlaka kutoruhusiwa kukusanya Ada na Tozo ya Mafuta yanayoingia nchini:** ZMA kwa mujibu wa Kanuni ya Ada na Tozo ya mwaka 2012, imepewa uwezo wa kukusanya ada ya shilingi 6.9 kwa kila lita ya mafuta nchini. Lengo la tozo hiyo ni kuisaidia Mamlaka kuendesha shughuli mbali mbali ikiwemo mafunzo kwa mabaharia, shughuli za uhifadhi, utafutaji na uokozi. Hata hivyo, hadi Kamati inakusanya taarifa hizi Mamlaka haijaruhusiwa kukusanya ada na tozo hiyo.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara iendelee kufanya mazungumzo na TCRA ili iweze kuipatia ZMA CALL SIGN kwa wakati ili shughuli za usajili wa meli za kimataifa zifanyike kwa wakati.

2) Kamati inaishauri Mamlaka na Wizara kwa Ujumla kuendelea kufuatilia ruhusa ya kukusanya ada ya mafuta kwa mujibu wa Kanuni ya Ada na Tozo, mwaka 2012.

3) Pamoja na ahadi ya Serikali ya kutafuta Usafiri wa Umma wa Majini, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuweka mazingira mazuri ili kuwavutia wawekezaji kuleta vyombo vya kisasa vitakavyosaidia kutoa huduma kwa wananchi wa Unguja, Pemba na Tanga.

4) Mamlaka ihakikishe vyombo vyote vya majini vinavyopakia abiria vinatoa matangazo na kuwatambua abiria wote wenye mahitaji maalum kabla ya safari kwa ajili ya kuwawekea uangalizi maalum ikiwa ni miongoni mwa tahadhari ya kujikinga na maafa yanayoweza kujitokeza.

**2:9 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR**

Taasisi nyengine inayounda Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ni Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, ambayo kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2023, imefanikiwa kuimarisha huduma za ulinzi na usalama katika Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa kuvifanyia matengenezo vifaa vya ulinzi na usalama ikiwemo mashine 10 za ukaguzi zimefanyiwa "service" na mashine mbili zimefanyiwa matengenezo makubwa Unguja na Pemba. Pia, Kamati iliarifiwa kwamba Mamlaka imefanikiwa kutoa mafunzo ya ulinzi na usalama kwa wafanyakazi 67 kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa Viwanja vya Ndege Unguja na Pemba.

Aidha, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kufanya matengenezo mbalimbali katika majengo ikiwemo mapaa yanayovuja katika jengo la Terminal 2, kubadilisha tiles na kuweka mpya, kupaka rangi nje na ndani, kukiboresha kituo cha Polisi AAKIA pamoja na kukiwekea miundombinu ya Tehama. Pia, matayarisho ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa jengo jipya la TB 2 la AAKIA yanaendelea. Vilevile, matengenezo makubwa yamefanyika katika njia ya kupitia ndege (Taxiway C) katika maeneo ya "shoulder" kwa kuiongezea ubora barabara hiyo.

Vile vile, Kamati imebaini kwamba kwa upande wa huduma za ndege na abiria, Mamlaka imefanikiwa kuhudumia ndege za ndani 28,199, Ndege za nje 7,053 pamoja na kuhudumia tani za mizigo 1,932. Aidha, jumla ya abiria wa ndani 456,121 pamoja na abiria wa nje 652,684 wamehudumiwa katika kipindi hicho.

**Changamoto za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar**

a) Uchakavu wa miundombinu katika jengo la abiria TB2 AAKIA.
b) Ukosefu wa elimu ya huduma kwa wateja kwa baadhi ya watoa huduma katika viwanja vya ndege.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara ihakikisha inawapatia mafunzo ya Huduma kwa Wateja (Customer care) kwa wafanyakazi wote wanaotoa huduma katika Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

2) Wizara isimamie ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege na kukagua miundombinu hiyo ili kujua hitilafu mapema na kuzirekebisha kwa kuimarisha mazingira mazuri na kutunza haiba ya viwanja vyetu kuzidi kuvutia kimataifa.

## 2:10 IDARA YA MAWASILIANO

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, Wizara kupitia Idara ya Mawasiliano katika kuimarisha huduma za TEHAMA Zanzibar imefanikiwa kutoa mafunzo ya uelewa wa TEHAMA kwa wananchi kupitia vituo vya TEHAMA jamii ambapo jumla ya wananchi wapatoa 814 walipata mafunzo hayo Unguja na Pemba.

## 2:11 SHIRIKA LA MAWASILIANO ZANZIBAR (ZICTIA)

Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, Wizara kupitia Shirika la Mawasiliano katika kuimarisha huduma za TEHAMA Zanzibar imefanikiwa kuzifanyia matengenezo kilomita 8 za Mkonga katika kisiwa cha Unguja. Aidha, ZICTIA imepiga hatua kwa kuviunganisha na Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano vituo (21) vya taasisi mbalimbali Unguja na Pemba na kuanza mazungumzo na SJMT kuona namna ya kupata ufadhili wa Mradi husika kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidigitali.

Pia, ZICTIA imefanikiwa kusaini Mkataba na Kampuni ya Tigo/Zantel kwa lengo la kufanya Upembuzi yakinifu/Tafiti kwa ajili ya huduma ya kufikisha mkonga majumbani.

Kwa upande wa kituo cha kuhifadhia kumbukumbu za kielektroiki (Data Center), jumla ya mifumo 13 mipya kutoka taasisi mbalimbali imehifadhiwa katika kituo hicho kwa kipindi cha miezi sita.

## 2:12 WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2023, Wakala wa Majengo imefanikiwa kuandaa nyaraka 12 za ujenzi pamoja na BOQ kwa Unguja na 4 Pemba. Sambamba na hayo, Wakala wa Majengo umefanikiwa kusimamia miradi ya ujenzi 24 Unguja na 16 Pemba pamoja na kufanya ukaguzi na tathmini za nyumba za Wakala wa Majengo 7 Unguja na Pemba.

### Changamoto za Wakala wa Majengo Zanzibar

a) Wakala bado anakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa fedha za kutekelezea majukumu waliyojipangia.
b) Wakala kukabidhiwa nyumba za Serikali ambazo ni chakavu zinazohitaji matengenezo makubwa.
c) Upungufu wa vitendea kazi pamoja na teknolojia za kisasa.
d) Miradi mingi ya Serikali bado inaendelea bila ya kupitia kwa Wakala wa Majengo Serikali.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaebdelea kuishauri Serikali kupitia Wizara kuwapatia fedha katika bajeti ili waweze kutekeleza majukumu yao.
2) Kamati inaendelea kutoa wito kwa Serikali kuwatumia Wakala wa Majengo katika miradi yao ili waweze kutoa ushauri wa kiutaalamu na kuweza kusaidia kufanikiwa kwa miradi hiyo kwa ubora zaidi.

## 2:13 BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI NA WAKADIRIAJI MAJENGO

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara katika kipindi cha Julai – Disemba, 2023, Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo imefanikiwa kusajili wataalamu 38 wa ujenzi pamoja na kusajili miradi ya ujenzi inayosimamiwa na wataalamu 128 Unguja na Pemba. Pia, Bodi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi 66 iliyotekelezwa na Wataalamu ambao wamewasajili.

### Changamoto za Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo

Pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kwamba bado Bodi hii inaendelea kukabiliwa na baadhi ya changamoto ikiwemo; -

a) Baadhi ya wataalamu wa kigeni kutojisajili hasa wale wanaofanya kazi katika Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo jambo ambalo ni kosa kisheria.
b) Wataalamu waliojisajili kuchelewa kulipa ada ya mwaka.
c) Ukosefu wa watendaji wa kudumu kunakopelekea kupungua kasi ya utendaji kazi.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha Wataalamu wote wazawa na wale wa Kigeni wanasajiliwa kama ilivyoelekezwa katika sheria zilizopo.
2) Bodi ihakikishe inasimamia ipasavyo suala la ulipaji wa ada kwa Wakandarasi wote waliosajiliwa ikiwa ni njia moja wapo ya kuongeza mapato ya Serikali.

## 2:14 BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI ZANZIBAR

Kamati iliripotiwa kwamba kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, Wizara kupitia Bodi hii imefanikiwa kusajili wakandarasi wapya waujenzi 29 pamoja na kuwafanyia ukaguzi wakandarasi hao. Aidha, Bodi imesajili miradi 113 ya ujenzi inayosimamiwa na Wakandarasi Unguja na Pemba.

### Changamoto za Bodi ya Usajili wa Wakandarasi

Kamati imebaini kwamba bado Bodi hii nayo inaendelea kukabiliwa na baadhi ya changamoto ikiwemo; -

a) Kuendelea kukosa mashirikiano kwa baadhi ya Taasisi za Serikali kusajili miradi yao.
b) Uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi jambo linapelekea Bodi kufanya ukaguzi na kupunguza mapato kwa Serikali.
c) Mapato yote yanayokusanywa na Bodi yanaingia katika Mfuko wa Hazina jambo ambalo linapelekea Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati kwani fedha za matumizi ya Bodi huwa hazipatikani kama inavyo hitajika.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara iendelee kuhimiza mashirikiano kwa baadhi ya Taasisi za Serikali kusajili miradi yao kama taratibu zinavyoelekeza.

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI**

## 3:0 UTANGULIZI

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar imeanzishwa kwa Lengo la kusimamia utekelezaji wa Sera pamoja na Sheria mbali mbali zinazohusiana na masuala ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makaazi.

## 3:1 MUUNDO WA WIZARA

Kimuundo Wizara hii inajumuisha sekta tatu ambazo ni mipango na Uendeshaji, Ardhi pamoja na Makaazi ambapo sekta hizi ni za utoaji wa huduma kwa jamii. Kiutendaji sekta hizi zimegawika katika Taasisi saba na Bodi Tendaji mbili kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| | **SEKTA YA MIPANGO NA UENDESHAJI** | |
| 1. | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | Inaongozwa na Mkurugenzi |
| 2. | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | Inaongozwa na Mkurugenzi |
| 3. | Ofisi ya Mdhamin Pemba | Inaongozwa na Afisa Mdhamini |
| | **SEKTA YA ARDHI** | |
| 4. | Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali | Inaongozwa na Mthamini Mkuu wa Serikali |
| 5. | Mahkama ya Ardhi | Inaongozwa na Mwenyekiti |
| 6. | Kamisheni ya Ardhi (CoLA) | Inaongozwa na katibu Mtendaji |
| | **SEKTA YA MAKAAZI** | |
| 7. | Shirika la Nyumba | Linaongozwa na Mkurugenzi Mkuu |
| 8. | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba | Inaongozwa na Mwenyekiti |
| 9. | Bodi ya Kondominio | Inaongozwa na Mwenyekiti |
| 10 | Idara ya Maendeleo ya Makaazi | Inaongozwa na Mkurugenzi |

### 3:2 SEKTA YA ARDHI

Sekta hii inaundwa na Kamisheni ya Ardhi, Mahakama ya Ardhi na Afisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ambapo ina jukumu la kuhakikisha usalama wa matumizi ya ardhi na umiliki (Secure of land Tenure) kwa wananchi.

### 3:2:1 KAMISHENI YA ARDHI

Hadi kufikia Disemba 2023, Kamisheni ya Ardhi imefanikiwa kutekeleza majukumu ya katika nyanja tofauti, miongoni mwa mafanikio yake ni kama ifuatavyo: -

1. Jumla ya hati za haki ya matumizi ya Ardhi 575 zimetayarishwa (418 kwa Unguja na hati 157 kwa Pemba).
2. Kuendelea na zoezi la Utambuzi katika maeneo ya Mbweni kwa Unguja na Utaani kwa Pemba ambao upo katika hatua za uwekaji wa majina hadharani (Public Display).
3. Kamisheni imefanikiwa kupima viwanja 1,129 (561 Unguja na 568 Pemba). Maeneo yaliyopimwa ni maeneo ya makaazi, taasisi, mashamba, eka na maeneo ya vitega uchumi.
4. Jumla ya ramani 1,367 (1,122 Unguja na 245 kwa Pemba) zimetayarishwa**.**
5. Jumla ya maeneo 404 ya uhaulishaji yamekaguliwa pamoja na kufanya ziara katika maeneo Saba (7) yaliyogundulika na changamoto katika uhaulishaji.
6. Imeandaa Miongozo 527 (396 Unguja na 131 Pemba) kwa ajili ya upangaji na usimamizi wa Maendeleo ya Miji. Aidha, **z**oezi la upangaji, usimamizi na uendelezaji wa maeneo ya Kibuteni kwa Unguja na Furaha Pemba limeaanza, ambapo kwa eneo la Furaha lipo katika hatua ya kukamilisha ramani ya mpango wa matumizi ya Ardhi na kwa eneo la Kibuteni lipo katika hatua ya kutambua mipaka ya eneo.
7. Kwa hatua za awali, Kamisheni imefanikiwa kuyapanga Maeneo matatu (3); mawili (2) Unguja ambayo ni Fumba na Nyamanzi na eneo moja (1) la Makangale (Mji wa Utalii) kwa Pemba.

**Changamoto za Kamisheni ya Ardhi**

a) Uhaba na uchakavu wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya kusimamia utekelezaji na ufuatiliaji wa shughuli zilizopangwa.
b) Uhaba wa vifaa na wataalamu kwa Sekta ya Ardhi.
c) Kiwango kidogo cha uelewa wa jamii juu ya dhana ya utawala na usimamizi wa Ardhi.
d) Kuendelea kuwepo Ardhi kubwa ambayo bado haijafanyiwa utambuzi na kusajiliwa kulingana na malengo ya usajili.
e) Uvamizi wa maeneo kwa matumizi tofauti na yale yaliyoainishwa katika mipango mikuu ya matumizi ya ardhi kama vile maeneo ya miundombinu, kilimo na hifadhi za misitu.
f) Pia, uvamizi katika maeneo ya wazi (open spaces), hifadhi ya barabara (Road reserve), viwanja vya michezo pamoja na fukwe.
g) Ukosefu mkubwa wa Mipango Miji na Vijiji, suala ambalo linapelekea ujenzi holela na kusababisha changamoto nyengine ya ugumu wa kupeleka huduma za kijamii ikiwemo barabara, mifumo ya maji safi na maji machafu na Zimamoto.
h) Mazingira ya kazi hayaridhishi na kutokidhi mahitaji ya Kamisheni ya Ardhi (Majengo ya Kamisheni Unguja na Pemba).

**MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaiomba Serikali kulipitia na kulifanyia kazi andiko la mradi wa jengo ulioandaliwa na Kamisheni ya Ardhi ambalo litajumuisha Taasisi zote za Kamisheni ya Ardhi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa urahisi.
2) Kamati inaishauri Kamisheni na Wizara kwa ujumla kufuatilia Serikalini kupitia Tume ya Utumishi wa Umma suala la upatikanaji wa vibali vya ajira katika fani zenye mahitaji mahsusi (rare study) ili waweze kutekeleza majukumu kwa ufanisi zaidi.
3) Kamati inaiomba Kamisheni ya Ardhi kufuatilia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuhakikisha vifaa muhimu katika sekta hii ya Ardhi vinapatikana kwa wakati ili

mipango ya Serikali ipate kufanikiwa kwa ubora, kiwango kinachohijika, na kwa wakati.

4) Kamati inaishauri Kamisheni kutanua wigo na kutumia njia tofauti katika kutoa elimu kwa jamii juu ya masuala ya ardhi.
5) Kamati inaitaka Idara ya Mipango Miji na Vijiji kupitia Kamisheni ya Ardhi kuendelea na zoezi la upimaji ardhi katika maeneo tofauti mbali na yale ya Kilimo kwa Pemba na Uwekezaji Unguja.
6) Kamati inashauri kwamba utaratibu ulioanzishwa wa uwekaji wa Miji Mipya uende sambamba na ushirikishwaji wa taasisi zote zinazohusika na uwekaji wa miundombinu ili huduma za kijamii zifikishwe mapema na kwa uharaka katika maeneo husika kwa ajili ya kuepusha usumbufu wa kimiundombinu na kimazingira unaoweza kujitokeza hapo baadae.
7) Kamisheni ifanye Kampeni maalum katika taasisi za kielimu kwa lengo la kushawishi vijana wa jinsia zote kusoma fani mbali mbali za kitaalamu zinazohusiana na masuala ya Ardhi ili kupunguza tatizo la wataalamu katika sekta ya Ardhi.

### 3:2:2 MAHKAMA YA ARDHI.

Mahkama ya Ardhi Zanzibar imeendelea na jukumu lake la msingi la kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri ya Migogoro ya Ardhi yanayowasilishwa na wananchi pamoja na taasisi mbalimbali kuhusiana na masuala ya ardhi nchini. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, Mahkama ya Ardhi imepokea jumla ya kesi mpya mia moja na nne (104) ambazo zimefunguliwa Unguja na Pemba. Aidha, Mahkama imeendelea kusikiliza kesi hizo pamoja na za awali ambapo kesi sabini na saba (77) zimetolewa maamuzi, sawa na wastani wa asilimia 47 ya lengo la kuamua kesi 165 kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023, kama mchanganuo ufuatao unavyoonyesha hapo chini: -

| SN | MKOA HUSIKA | KESI MPYA ZILIZOPOKELEWA | KESI ZILIZOTOLEWA MAAMUZI | KESI ZINAZOENDELEA MAHAKAMANI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | MJINI MAGHARIBI | 28 | 17 | 83 |
| 2 | KASKAZINI UNGUJA | 10 | 11 | 29 |
| 3 | KUSINI UNGUJA | 22 | 11 | 41 |
| 4 | KASKAZINI PEMBA | 20 | 16 | 21 |
| 5 | KUSINI PEMBA | 24 | 22 | 42 |
| | **JUMLA KUU** | **104** | **77** | **216** |

**Changamoto za Mahkama ya Ardhi**

a) Mahakama inakabiliwa na changamoto ya uingizwaji wa kifedha jambo ambalo linakwaza kutotekelezeka kwa shughuli ambazo imejipangia katika mpangokazi wake.
b) Ucheleweshaji wa Kutolewa maamuzi ya kesi zinazohusu migogoro ya Ardhi.

**MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1. Kamati inaiomba Wizara ya Fedha na Mipango kulitafutia ufumbuzi suala la upatikanaji wa fedha kwa Mahkama ya Ardhi ili waweze kutekeleza majukumu yao waliopangiwa.
2. Kamati inaishauri Mahkama ya Ardhi kujikita katika matumizi ya njia ya usuluhishi wa kutatua migogoro ili kuwapunguzia wananchi gharama na muda wa kufuatilia mashauri Mahkamani.
3. Kamati inasisitiza kwa viongozi mbali mbali kuacha tabia ya kuingilia kesi pale ambapo Mahkama, na zile ambazo tayari Mahakama imeshatoa maamuzi, kwani kufanya hivyo ni kuingilia uhuru wa Mahkama na ni kosa kisheria ambapo wakati mwegine husababisha kuibuka kwa migogoro mingine mipya katika jamii.

### 3:2:3 OFISI YA MTHAMINI MKUU WA SERIKALI.

Ofisi imeanzishwa kwa Sheria ya usajili wa Wathamini Nambari 5 ya mwaka 2015 kwa madhumuni ya kuhakikisha usimamizi mzuri wa uthaminishaji rasilimali kwa malengo mbali mbali ya Sekta ya Umma, Biashara na Wananchi kwa ujumla. Kazi kuu ya mthamini mkuu ni kuthibitisha kazi za uthamini zinazofanywa nchini na Wathamini wa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi. Kamati ilifanya mahojiano na Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali na kubaini kwamba kwa kipindi cha Julai hadi Disemba, 2023, Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali imetekeleza shughuli zifuatazo: -

1. Jumla ya ripoti 295 zimethibitishwa na Mthamini Mkuu ambapo kati ya hizo, 87 ni ripoti za fidia, 12 ripoti za mikopo, 111 ripoti za uthamini kwa ajili ya thamani, 83 ripoti ya uthamini wa mirathi na 2 uthamini kwa ajili ya uhaulishaji.
2. Ofisi imeandaa rasimu za miongozo mbalimbali ya uthamini ikiwemo:
    - Rasimu ya Muongozo wa Uthamini wa Fidia.
    - Rasimu ya Muongozo wa Masafa ya Miti na Mazao (Trees and Crops spacing).
    - Rasimu ya viwango vya Thamani za Ujenzi.
    - Rasimu ya Muongozo wa Haki ya Matumizi ya Ardhi (Land rates).
    - Marekebisho ya Thamani za Miti na Mazao.
    - Wajibu wa wadau katika uthamini wa fidia.

Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba miongozo hiyo ipo katika hatua mbalimbali za kujadiliwa na Wadau kwa ajili ya kupata maoni yao.

3. Ofisi ilikutana na Uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa ajili ya kuwasilisha Rasimu ya Muongozo wa Fidia na kupata maoni yao. Pia, Rasimu ya Muongozo wa Masafa ya Miti na Mazao (trees and crops spacing) umeshatayarishwa na unasubiri maoni ya wadau ili kuboreshwa zaidi.

**Hali ya Madeni**

Kamati imebaini kwamba hadi kufikia Disemba 2023, Ofisi ya Mtathmini Mkuu inadai kiasi ya Shilingi **350,052,696** kwa taasisi mbali mbali ambazo bado hazijalipa ada ya shughuli za Uthamini kama ifuatavyo: -

**Madeni ya Taasisi ambazo hazijalipa ada ya uthamini hadi kufikia Disemba, 2023.**

| NAMB. | TAASISI | DENI |
|---|---|---|
| 1 | UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM | 26,953,000 |
| 2 | MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI (ZPRA) | 1,392,000 |
| 3 | SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC) | 9,957,000 |
| 4 | BARAZA LA MANISPA MAGHARIBI A | 300,273,000 |
| 5 | AMINA AHMED MOHAMED RAKGAS Z. LIMITED | 4,177,000 |
| 6 | VILLA TULIA | 3,123,696 |
| 7 | JAFER HAMAD CHILALA | 4,177,000 |
| **JUMLA** | | **350,052,696** |

*Chanzo Ofisi ya Mtathmini Mkuu, 2023.*

**Changamoto za Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali.**

a) **Uhaba wa Wataalamu wa fani ya Uthamini.** Kamati imebaini kwamba Changamoto hii inatokana na uwepo wa Miradi mingi na mikubwa ya Maendeleo inayotekelezwa nchini ikiwemo Miradi ya Barabara, maji, umeme na Bandari inayopelekea ongezeko la mahitaji makubwa ya wataalamu hao.

b) **Uhaba wa upatikanaji wa fedha za kuendesha Ofisi.** Ambapo Ofisi kwa sasa imekodi jengo la Michenzani Mall ambapo inashindwa kulipa kodi ya jengo hilo kwa wakati kutokana na upatikanaji mdogo wa fedha za kuendesha Ofisi.

**c) Kukosekana kwa mfumo wa kisasa (kidigitali) wa kuhifadhia taarifa na ripoti za uthamini zinazofanywa na Ofisi.**

**MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaihimiza Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kutekeleza Miradi inayoletwa kupitia Taasisi mbali mbali kwa haraka ili kuzuia Miradi kuchelewa kuanza utekelezaji.
2) Kamati inaishauri Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali kupitia vizuri tathmini zao ili kupunguza lawama kwa wananchi wasioridhika na tathmini ya maeneo yao.
3) Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Mthamini Mkuu wa Serikali ipatiwe nguvu ya rasilimali fedha pamoja na rasilimali watu ili iweze kufanya kazi zake kwa uweledi.
4) Kamati inasisitiza Wizara ya Ardhi kuharakisha kupatikana kwa Rasimu za miongozo mbali mbali ya uthamini Zanzibar.

**3:3 SEKTA YA MAKAAZI**

Sekta hii inaundwa na Idara ya Maendeleo ya Makaazi, Shirika la Nyumba, Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba na Bodi ya Kondominio ambapo jukumu la sekta hii ni kuhakikisha upatikanaji wa Makaazi salama na endelevu kwa wananchi pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wa sekta binfsi katika huduma za makaazi

**3:3:1 IDARA YA MAENDELEO YA MAKAAZI**

Idara ya Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kusimamia suala la Makaazi pamoja na kusajili, kuratibu matumizi pamoja na majengo yenye sehemu zinazomilikiwa na watu tofauti ikiwemo majengo ya ghorofa. Hadi Disemba, 2023, Idara ya Maendeleo ya Makaazi imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

1. Inaendelea na hatua za usajili wa Kondominio kwa Unguja na Pemba. Ofisi imetoa jumla ya fomu Mia Moja (100) za maombi ya usajili wa Kondominio.
2. Imefanya usajili wa Ramani Tano (5) katika miradi ya Kondominio ambayo ni Furaha Investment Limited uliopo Bwejuu, Dream Company Limited (Phase 1) uliopo Nungwi, Mwerevu Company Limited uliopo Michamvi, Johari Developers Limited uliopo Kizimkazi na PGH Company Limited uliopo Jambiani.

3. Imefanya ukaguzi kwenye jumla ya Miradi tisa (9) kabla ya kusajiliwa ili kuhakikisha kuwa imekidhi vigezo vya kusajiliwa. Miradi hiyo iliyokaguliwa ikiwemo miradi ya Mbweni, Nungwi, Kizimkazi, Paje, Kilimani na Michenzani kwa Unguja na Mapinduzi (Uweleni) Ng'ombeni na Uweleni Mkoani Pemba.
4. Imeendelea kufanya uchambuzi na uhakiki wa maombi mbali mbali ya usajili kupitia kamati maalum, jumla ya maombi tisiini na mbili (92) yamehakikiwa. Uhakiki huu unafanywa kwa kushirikiana na Masheha wa Shehia husika.

**Changamoto za Idara ya Maendeleo ya Makaazi**

a) Uchache wa Rasilimali watu pamoja na Vitendea kazi.
b) Kukosekana kwa usafiri wa kufanya ufuatiliaji wa Miradi ya Kondominio.
c) Kuwepo kwa Miradi ya Kondominio inayotekelezwa na Taasisi za Serikali ambayo haifuati taratibu za usajili wa Kondominio kwa mujibu wa Sheria.
d) Kuwepo kwa maombi mengi ambayo yanahitaji kupatikana kwa ithibati za Mirathi.

**MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaishauri Wizara kuwasiliana na kila Taasisi yenye Miradi ya Kondominio kuhakikisha inafuata taratibu za usajili wa Kondominio kwa mujibu wa Sheria.
2) Wizara iongeze kasi ya kushughulikia maombi ya ithibati za Mirathi ili kupunguza mrundikano wa maombi ya ithibati.

### 3:3:2 SHIRIKA LA NYUMBA

Shirika la Nyumba ni taasisi inayojitegemea ambayo imeanzishwa chini ya Sheria namba 6 ya mwaka, 2014. Kupitia Sheria hii, Shirika limepewa mamlaka ya kusimamia na kuendeleza sekta ya nyumba Zanzibar kwa lengo la kuongeza pato la Taifa na kuwapatia wananchi makaazi bora na endelevu.

**MAFANIKIO YA SHIRIKA LA NYUMBA**

Kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2023 Shirika limefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

1) Ujenzi wa majengo manne yenye nyumba 72 za Makaazi na maeneo ya biashara Mombasa (Kwa Mchina) unaendelea kwa hatua za upigaji plasta. Mkandarasi wa ujenzi huo ni Kampuni ya Simba Developer na Mshauri Elekezi ni Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA). Kwa ujumla kazi hiyo ya ujenzi imefikia asilimia 50%.
2) Ujenzi wa jengo nambari 1293/1294 la Darajani lenye ghorofa tatu unaendelea ambapo kazi zilizofanyika ni ujenzi wa 'formwork' za sakafu ya tatu na ujenzi wa kuta za mawe na tofali kwa ghorofa ya kwanza. Kazi hiyo ya ujenzi inafanywa na kusimamiwa na Shirika lenyewe ambapo imefikia asilimia 47%.
3) Matengenezo ya awamu ya pili (phase II) ya nyumba nambari 1699/1705 Mkunazini (Mnadani) yanaendelea kwa kazi za uvunjaji na ujengaji wa kuta za mawe na tofali. Kazi hiyo ya ujenzi inafanywa na kusimamiwa na Shirika lenyewe na ujenzi huo umefikia asilimia 27 ya kukamilika.
4) Kazi ya utayarishaji wa miradi mipya ya shirika imefanyika ambapo michoro ya miradi iliyoandaliwa ni mradi wa nyumba za makaazi Nyamanzi, mradi wa nyumba za makaazi na biashara Kisakasaka kwa Unguja na mradi wa nyumba za makaazi na biashara Mfikiwa, Chake chake Pemba.
5) Ujenzi wa jengo la ghorofa nne la biashara na makaazi Mkungu Malofa (Mabatini) Chake chake - Pemba unaendelea ambapo kazi ya kusuka nondo na kumwaga zege ya columns katika ghorofa ya pili inaendelea. Kazi hiyo inafanywa na shirika na kusimamiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 45 kukamilika.
6) Matayarisho kwa ajili ya Matengenezo ya kuezeka nyumba namba ZHC19/02A-D Tibirinzi yamefanyika.
7) Kazi za ujenzi wa jengo la Ofisi za Shirika la Nyumba Pemba iliyopo Machomane imeanza kwa hatua za awali zikiwemo uvunjaji wa jengo lililopo, uondoshaji kifusi, kazi ya ujenzi wa msingi na uekaji wa uzio (fencing).

8) Matengenezo ya Ofisi za Shirika Micheweni Pemba yamekamilika na huduma za kiofisi zimeshaanza kutolewa kwa wapangaji wa Wilaya ya Micheweni.
9) Matayarisho ya mradi wa Mfikiwa Chake chake - Pemba yanaendelea. Aidha, kazi ya uchunguzi wa udongo (Soil test) katika eneo la Mfikiwa inaendelea na Shirika tayari limekabidhiwa ripoti kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TCAA) kuhusu taratibu za ujenzi katika eneo hilo.
10) Kazi za uzibuaji na usafishaji wa makaro ya maji machafu zimefanyika katika Nyumba za Maendeleo za Polisi Line, Madungu, Machomane na Mtemani.

**Ukaguzi wa Kamati katika Miradi ya Shirika la Nyumba Pemba**

- **Ofisi za Shirika Micheweni Pemba**
- **Matengenezo ya Nyumba ya Maendeleo Mtemani**

Kamati ilijuilishwa kwamba Shirika la Nyumba lilitumia jumla ya shilingi **21,378,000** kwa ajili ya Ukarabati wa Ofisi ya Shirika Micheweni ili iweze kutoa huduma kwa wapangaji wa Shirika katika Wilaya hiyo.

Wakati huo huo, Kamati ilitembelea Mradi wa Matengenezo ya Nyumba za Maendeleo Mtemani Wete uliotumia jumla ya Shilingi **121,468,100.** Aidha, Kamati ilitembelea Miradi hiyo kwa vipindi viwili mfululizo kwa nia ya kujiridhisha juu ya hatua ya ujenzi inayodaiwa kukamilika. Uchuguzi wa Kamati umebaini kwamba Ukarabati uliofanyika haulingani kabisa na thamani ya fedha iliyotumika (Value for Money).

**Hali ya Madeni ya Shirika la Nyumba**

Shirika hadi kufikia 31 Disemba, 2023 lilikuwa na jumla ya deni la **TZS 1,793,236,814** kutoka kwa wapangaji wake wote Unguja na Pemba ambapo **TZS 1,603,219,814** kwa upande wa Unguja na **TZS 190,017,000** kwa upande wa Pemba.

**Changamoto za Shirika la Nyumba**

a) Uchakavu wa nyumba za Shirika (Maaendeleo, Mji Mkongwe na Vijiji) kutokana na kukaa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo.
b) Kutokukidhi mahitaji ya nyumba na makaazi kwa Zanzibar kwa kuwa mahitaji halisi ya nyumba kwa sasa ni makubwa mno kulingana na uwezo mdogo wa Shirika wa kuweza kukidhi mahitaji hayo.

c) Uwepo wa deni kubwa na la muda mrefu la wapangaji wa nyumba za Shirika.
d) Kodi za nyumba ni ndogo ukilinganisha na gharama za matengenezo ya nyumba hizo jambo linalopelekea Shirika kushindwa kufanya matengenezo kwa kiwango kinachotakiwa.
e) Riba kubwa kutoka taasisi za kifedha ikiwemo mabenki ambapo Shirika linashindwa kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba mpya.

**MAAGIZO, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inawasihi Shirika la Nyumba katika ujenzi wa nyumba mpya na ukarabati wa nyumba zilizochoka wawe waadilifu katika gharama za ujenzi, umadhubuti wa vifaa na ubora wa kazi zenyewe kwani nyumba hizo ni tegemeo la Serikali katika kuimarisha makaazi kwa wananchi.
2) Kamati inaisisitiza Shirika la Nyumba kufuatilia kwa karibu juu ya mikakati iliyojiwekea ya kuhakikisha madeni yanalipwa kwa wapangaji wake wote, hasa kwa vile bado Shirika ni changa ambapo linahitaji mapato ili liweze kujiendesha kibiashara.
3) Kamati inalitaka Shirika la nyumba kufikiria kujenga makaazi ya wananchi wenye kipato cha chini, kwa kuwa imebaini gharama za nyumba nyingi zinazojengwa hivi sasa zinawalenga zaidi wananchi wenye kipato cha juu. Aidha, kamati inasisitiza mbali ya ujenzi wa nyumba hizo lakini Shirika liweke mkakati maalumu ambao utahakikisha nyumba hizo zinawafikia walengwa waliokusudiwa kama azma ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964 chini ya Mzee Abeid A. Karume inavyotuelekeza.
4) Kamati inaishauri Shirika la Nyumba la Zanzibar kuiga mfano wa Shirika la Nyumba la Tanzania (NHC) ambapo wanajenga nyumba nyingi na bora kwa ajili ya makaazi na kuwanufaisha wananchi wa kipato cha juu, kati na cha chini.

### 3:3:3 BODI YA KUDHIBITI KODI ZA NYUMBA

Bodi ya kudhibiti Kodi za Nyumba inajukumu la kupokea, kuratibu, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yanayofunguliwa ambayo yanahusiana na migogoro ya kodi za nyumba

***(mali zisizohamishika)*** Zanzibar. Hadi kufikia Disemba 2023, Bodi hii imetekeleza kazi zifuatazo:-

1. Imepokea mashauri Kumi na Saba (17), kati ya hayo Unguja Kumi na Sita (16) na Pemba Moja (1). Hivyo, kufanya Bodi hii kwa sasa kuwa na Mashauri 40.
2. Imesikiliza mashauri Ishirini na Nne (24) kwa kipindi hicho na imeyatolea maamuzi mashauri ya migogoro ya kodi za nyumba Kumi (10) kwa Unguja.

**Changamoto za Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba**

Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba inakabiliwa na Changamoto zifuatazo: -

a) Uhaba wa watendaji wa kufanikisha shughuli za Bodi.

b) Kukosekana kwa ukumbi wa kusikiliza mashauri ya Kodi za Nyumba Unguja na Pemba.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ifanye juhudi za kutafuta ukumbi au kuiwezesha Bodi hiyo kufanya shughuli zake kwa ufanisi zaidi ikiwemo kusikiliza mashauri ya Kodi za Nyumba.

## WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

### 4:0 MUUNDO WA WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

Wizara ya Maji, Nishati na Madini inaundwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Maendeleo ya Maji, Idara ya Nishati na Madini pamoja na Afisi Kuu – Pemba. Aidha Wizara hii ina Taasisi tatu ambazo ni Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO).

### 4:1 MALENGO YA WIZARA

Lengo kuu la Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutoa huduma nafuu, endelevu na zilizo bora kwa wananchi wote katika mazingira yanayofaa kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za maji, nishati na madini.

### 4:2 IDARA YA MAENDELEO YA MAJI

Idara ya Maendeleo ya Maji ina jukumu la kusimamia masuala yanayohusu sekta ya maji nchini. Kamati imeelezwa kwamba katika kipindi cha Julai – Disemba, 2023 Idara hii kwa kushirikiana na Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB) katika mwezi wa Julai 2023, imeandaa maabara ya kitaalamu “MINI DELIVERY LAB”, iliyolenga kujadili namna ya kuondoa changamoto za upatikanaji wa maji safi na salama kwa maeneo ya Unguja na Pemba.

Utafiti wa Kamati umebaini kwamba kikao hicho kilifanikiwa kuwasilisha mapendekezo mbali mbali yatakayosadia kufikia malengo ya Serikali ya kuhakikisha kuwa asilimia 95 ya wananchi wote wa Zanzibar wanapata maji safi na salama ifikapo mwaka 2025 ikiwemo;-

1. Kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa huduma za usambazaji wa maji safi na salama,
2. Kuongeza kasi katika kushughulikia tatizo la upotevu wa maji kabla ya kuwafikia walengwa,

3. Tathmini ya mageuzi ya kiuendeshaji ya ZAWA kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa kiuendeshaji katika utowaji wa huduma, uendeshaji kibiashara pamoja na kuziimarisha ofisi za maji za Wilaya kwa kuzipa uwezo wa kujitegemea na kujiendesha wenyewe.

Kwa Upande mwengie, Kamati imearifiwa kuhusu taarifa za matukio ya hali ya uvamizi katika maeneo mbalimbali ya hifadhi ya vianzio vya maji, ikiwemo vianzio vya maji katika mradi wa Exim-India hususani katika skimu ya Maungani-Dimani ambapo wananchi walivamia kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa makaazi ingawa baadae Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilichukua hatua za haraka za kulihami eneo hilo kwa kuweka mabango matano (5) yanayoonyesha kuwa ni sehemu ya hifadhi ya vianzio vya maji.

**Changamoto zinazoikabili Idara ya Maendeleo ya Maji**

a) Kukosekana kwa baadhi ya wataalamu wa sekta ya maji katika fani za; Ukadiriaji Majengo (Quantity Surveyor) na Fundi Umeme (Electrical Engineer).
b) Kukosekana kwa baadhi ya vifaa vya kiutendaji,
c) Kutokuwepo kwa mfumo wa usimamizi na ukaguzi wa vyanzo vya maji.
d) Kukosekana kwa miongozo ya kiutendaji katika utekelezaji wa baadhi ya majukumu ya Idara ikiwemo taarifa mbalimbali za sekta ya maji, muongozo wa Mashirikianao baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) katika Uwekezaji wa Sekta ya Maji.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaishauri Idara ya Maendeleo ya Maji kuandaa na kuwasilisha mahitaji ya rasilimali watu ya Idara kwa Uongozi wa Wizara kwa ajili ya kupatiwa wataalamu katika fani husika.
2) Kamati inashauri kuanzishwa kwa miongozo mbalimbali ambayo itasimamia utekelezaji wa sekta ya maji ikiwemo; muongozo wa Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) katika Uwekezaji wa Sekta ya Maji, na muongozo wa mgawanyiko wa kimajukumu kwa Taasisi zinazosimamia Sekta ya Maji.

3) Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuwa maeneo yote ya vianzio vya maji yawekwe mabango, uzio pamoja na kuimarisha hali ya ulinzi na usalama ili kuyahifadhi maeneo hayo.

### 4:3 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR (ZAWA)

Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imeanzishwa chini ya Sheria Namba 4 ya Mwaka 2006 kama ilivyopendekezwa katika Sera ya Maji ya Taifa ya Zanzibar ya Mwaka 2004, ikiwa na jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na kulinda na kuhifadhi rasilimali maji.

**Hali Halisi ya Uzalishaji wa Maji**

Wizara kupitia ZAWA katika kuendelea na jitihada za kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inaendelea kuimarika katika maeneo tofauti Unguja na Pemba, ZAWA imefanikiwa kuongeza uzalishaji wa maji ambapo hadi Disemba, 2023, hali ya uzalishaji maji imefikia wastani wa asilimia 70 kwa Unguja na Pemba, ambapo mahitaji ni Lita **275,980,481** kwa siku, uzalishaji ni lita **191,959,675** kwa siku, na mapungufu ni lita **84,020,806.**

***Jadweli 1: Mahitaji, uzalishaji pamoja na mapungufu kwa Unguja na Pemba***

| NA | MKOA | Mahitaji ya maji (lita kwa siku) | Uzalishaji wa maji (Lita kwa siku) | Mapungufu (Lita kwa siku) | Asilimia ya uzalishaji (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mjini Magharibi | 125,043,660 | 94,027,280 | 31,016,380 | 75 |
| 2. | Kaskazini Unguja | 36,020,600 | 24,323,500 | 11,697,100 | 68 |
| 3. | Kusini Unguja | 27,422,220 | 17,310,348 | 10,111,872 | 63 |
| 4. | Kaskazini Pemba | 43,806,651 | 25,453,747 | 18,352,904 | 58 |
| 5. | Kusini Pemba | 43,687,350 | 30,844,800 | 12,842,550 | 71 |
| | **JUMLA KUU** | **275,980,481** | **191,959,675** | **84,020,806** | **70** |

***Chanzo: ZAWA,2023***

### Hali Halisi ya Upotevu wa Maji

Kamati imebaini kwamba katika jitihada za kuzuia upotevu wa maji unaotokana na kupasuka kwa mabomba ya maji. Jumla ya mivujo 882 imezibwa katika wilaya tofauti za Unguja na Pemba. Kadhalika, ZAWA inaendelea kubadilisha mabomba chakavu na kulaza mabomba mapya ambayo kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi ya mivujo na upotevu wa maji badala yake maji mengi zaidi yataweza kuwafikia wananchi kama ilivyokusudiwa.

***Jadweli 2: linaonesha kazi ya uzibaji mivujo***

| Nam. | WILAYA | IDADI |
|---|---|---|
| 1. | Kaskazini –A | 22 |
| 2. | Kazkazini –B | 16 |
| 3. | Mgharibi A | 81 |
| 4. | Mgharibi B | 168 |
| 5. | Wilaya ya Mjini | 155 |
| 6. | Wilaya ya kati | 25 |
| 7. | Wilaya ya kusini | 43 |
| 8. | Wete | 74 |
| 9. | Micheweni | 148 |
| 10. | Chake- chake | 120 |
| 11. | Mkoani | 30 |
| **JUMLA** | | **882** |

*Chanzo: ZAWA, 2023*

### Hali ya Madeni ya Wateja wa ZAWA

Kamati imebaini kwamba hadi kufikia Disemba, 2023 ZAWA ilikuwa inadai jumla ya **TZS Bilioni 2,956,264,239.98** kutoka kwa wateja wake Unguja na Pemba kama inavyoonekana katika jedweli lifuatalo; -

***Jadweli 3: Madeni ya wateja wa ZAWA hadi Disemba, 2023.***

| NAM. | AINA YA WATEJA | IDADI | DENI |
|---|---|---|---|
| 1. | Wateja wa Majumbani | **125,214** | |
| 2. | Wateja wa Biashara | **1,487** | |
| 3. | Wateja wa Taasisi | **1,480** | |
| 4. | Wateja wa kilimo | **298** | |
| **JUMLA** | | **128,476** | **2,956,264,239.98** |

*Chanzo: ZAWA, 2023*

**Changamoto zinazoikabili ZAWA**

Katika kutekeleza majukumu yake ZAWA inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo: -

a) Uhaba wa wataalamu katika fani za Uhandisi.

b) Kupanda na kushuka kwa umeme mara kwa mara kunakopelekea hitilafu za kuungua pampu na vifaa katika visima.

c) Uchakavu wa miundombinu ya maji hususan bomba za Asbestos cement (AC) na uPVC.

d) Kuendelea kukosekana kwa hatimiliki katika maeneo ya vianzio vya maji.

e) Uvamizi wa maeneo ya vianzio vya maji pamoja na hujuma za miundombinu ya maji.

f) Ongezeko kubwa la vianzio na miundombinu ya maji linalopelekea Mamlaka ya Maji kuhitaji wafanyakazi wengi kusimamia.

g) Uharibifu wa mitandao/bomba unaosababishwa na ujenzi wa miundombinu ya barabara unaoendelea katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba, hali ambayo inarudisha nyuma jitihada za Mamlaka ya Maji ya kuimarisha huduma ya maji kwa wananchi wa Zanzibar.

h) Kamati imebaini kwamba mfumo wa maji wa ZAWA (Network) bado haufahamiki vizuri hata kwa wataalamu wenyewe na kwa wananchi kwa ujumla hivyo, husababisha uharibifu wa mara kwa mara katika sehemu zilizopita mabomba ya maji kunakotokana na harakati mbali mbali za kijamii pamoja na zile za kimaendeleo.

i) Kukosekana kwa elimu ya uchimbaji visima na utibabu wa maji suala ambalo linawapelekea wananchi kufanya shughuli hizo kiholela.

j) Kukosekana kwa takwimu, utambuzi pamoja na wamiliki wa visima binafsi vya maji.

k) Kukosekana kwa mfumo wa kuchanganua madeni ya Wadaiwa wa ZAWA kulingana na Makundi (Catagories) zao.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaiomba ZAWA kwa kushirikiana na Wizara kuendelea kuomba wataalamu kupitia OR - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ili kuweza kukidhi mahitaji na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi za Mamlaka.

2) Kamati inaisisitiza juu ya suala la kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji kwa kubadilisha bomba chakavu na kulaza mpya ili kuweza kuhuwisha huduma ya maji kuwa endelevu katika maeneo ya Unguja na Pemba.

3) Kamati inaendelea kuhimiza kuyahifadhi maeneo ya vianzio vya maji pamoja na miundombinu kwa kujenga uzio, kutafuta hatimiliki na kuweka ulinzi.

4) Kamati inaishauri ZAWA kufikiria kufunga vifaa maalum vya kudhibiti ongezeko la umeme ili kuepusha uunguaji wa pampu na vifaa mara kwa mara.

5) Kamati inashauri jitihada za ziada zizidi kuchukuliwa katika utambuzi wa mfumo wa maji wa ZAWA ikiwa ni njia moja wapo ya kuulinda na kuepukana na uharibifu wa mara kwa mara unaojitokeza.

6) Kamati inashauri kuwekwa utaratibu mzuri wa kitakwimu utakaowezesha kuwatambua wamiliki na idadi ya visima pamoja na matibabu ya maji ili kupunguza matumizi ya maji yasiyo salama na kuepusha mripuko wa maradhi katika jamii yetu.

7) Kamati inapendekeza kuharakishwa uwekwaji wa umeme hasa katika maeneo ya miradi mipya ya maji ili kuendana na matarajio ya kuanza kwa matumizi ya miradi hiyo.

8) Kamati inashauri ZAWA kufuatilia upatikanaji wa Hati Miliki ya meneo ya miradi ya maji kwa ujumla.

9) ZAWA iweke Mifumo Imara ambayo inaweza Kuchanganua Madeni ya Wateja wake kulingana na Makundi yaliyopo.

10) Kwa mara nyengine tena Kamati inaishauri Wizara kufuatilia ukamilishwaji wa suala la Malimbikizo ya Stahiki za Wafanyakazi wa ZAWA ambazo zimekwama Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais , Katiba, Sheria na Utumishi na Utawala Bora.

## 4:4 IDARA YA NISHATI NA MADINI

Idara ya Nishati na Madini ni moja kati ya Idara za Wizara ya Maji, Nishati na Madini ambayo ina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala yote yanayohusiana na Nishati na Madini. Idara imejigawa katika sekta ya Nishati na Sekta ya Madini.

### 4:4:1 Sekta ya Nishati

Sekta hii inajishughulisha na uratibu wa masuala yote ya nishati ikiwemo nishati mbadala, nishati ya kisasa, mafuta, gesi asilia, umeme pamoja na kutoa elimu juu ya matumizi ya nishati kwa jamii, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali.

**Baadhi ya Mafanikio katika Sekta ya Nishati**

Wizara imeendelea kushiriki Mikutano na Makongamano ya Kikanda na Kimataifa katika Masuala ya Nishati, mikutano hiyo inaibua fursa za kiuwekezaji na kitaalamu kwa watendaji katika kubuni vyanzo vipya vya nishati pamoja na kusimamia mikataba ya Sekta ya Nishati ya kitaifa na kimataifa. Miongoni mwa mafanikio ya Sekt ani Nishati ni haya yafuatayo: -

a) **Kuratibu Uingizaji wa Makaa Rafiki Zanzibar**: Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ipo katika utekelezaji wa Hati ya Makubaliano (MoU) baina ya Wizara na Wizara ya Madini Tanzania. Miongoni mwa mafanikio ya makubaliano hayo ni kuratibu uingizaji wa makaa rafiki na salama (Briquettes) kutoka Tanzania Bara kwa matumizi ya shughuli za kupikia na kuliomba shirika la STAMICO kufunga mtambo mmoja Zanzibar ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wananchi wa Zanzibar ikiwemo unafuu wa bei.

b) **Kutafuta vyanzo vya uzalishaji umeme:** Kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (ZECO) imeendelea na jitihada za kuhakikisha Zanzibar inapata vyanzo vyake vya ndani vya uzalishaji umeme pamoja na kuwepo kwa miundombinu imara ya kusafirisha na kusambaza umeme. Katika kulifanikisha suala hilo, tarehe 30/8/2023 Wizara imesaini Hati ya Makubaliano ya Mkataba (MoU) na Kampuni ya Grid X Africa yenye lengo la kuwekeza kwenye nishati ya jua kwa kiwango cha megawati 20, na uhifadhi wa betri kwa kiwango cha 20MWH. Aidha, Wizara imefanya majadiliano na jumla ya wawekezaji kumi na moja (11) walionyesha nia ya kuwekeza katika uzalishaji wa umeme kwa kutumia nishati ya jua, upepo, gesi, maji na taka.

c) **Kuimarisha miundombinu ya umeme:** Wizara imefanikiwa kuingia Mkataba na Kampuni ya Novavis kutoka nchini Marekani tarehe 25/7/2023. Mkataba huo una lengo la kuimarisha Gridi na kuondoa kasoro zinazosababisha kuwepo kwa tatizo la umeme mdogo na kukatika kwa umeme mara kwa mara. Mkataba huo utatekelezwa kwa kipindi cha miezi kumi na nane (18). Kwa hivi sasa, Kampuni hiyo ipo katika matayarisho ya kukamilisha manunuzi ya vifaa kwa ajili ya kuanza kazi ya ufungaji wa vifaa hivyo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

**Changamoto katika Sekta ya Nishati**

a) Wawekezaji wengi wenye nia ya kuwekeza kwenye sekta ya nishati hasa umeme wa upepo huitaka Wizara iingie makubaliano ya mauziano ya umeme (PPA)

katika hatua za awali kabla ya kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu. Jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya aina hiyo.

b) Kushindwa kutekeleza baadhi ya kazi kama zilivyoainishwa katika mpango kazi kutokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha za OC.

c) Kutokuwepo kwa Sheria ya Nishati ambayo ndiyo nyenzo kuu kwa Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini itayowezesha kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuzisimamia moja kwa moja Taasisi zilizopo chini ya Wizara, jambo ambalo linapelekea Taasisi hizo kufanya baadhi ya maamuzi bila ya Wizara kuwa na taarifa.

d) Uwepo wa tozo bandarini zinazozorotesha uingizaji wa makaa rafiki (briquettes) nchini kwa kupelekea bei ya bidhaa hiyo kua kubwa.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaishauri Wizara kuwasiliana na wadau wa maendeleo kusaidia kupitia tena utafiti wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo ili kukidhi haja ya mahitaji ya wananchi.

2) Wizara iendelee kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango katika kuhakikisha OC zinaingizwa kwa wakati na zenye kukidhi mahitaji halisi.

3) Kamati inasisitiza ipo haja ya ukamilishaji wa Sera ya Nishati, ambayo kukamilika kwake kutaiwezesha Wizara kuendelea na mchakato wa kuandaa Sheria ya Nishati.

4) Kamati inaiomba Wizara kukutana na Viongozi wakuu wa Wizara zinazohusika na tozo za uingizaji wa bidhaa ya makaa nchini ili kuangalia namna ya kuondoa changamoto hii.

### 4:4:2 Sekta ya Madini

Sekta hii inajishughulisha na uratibu wa masuala ya madini ikiwemo Maliasili Zisizorejesheka, uthaminishaji wa madini yanayoingia na kutoka nchini kwa lengo la kuhakikisha Serikali inapata mgao wake stahiki, pamoja na uratibu wa masuala mbalimbali ya kijiolojia.

**Mafanikio Katika Sekta ya Madini**

1) Kuanzisha mfumo wa uombaji wa madini kwa njia ya mtandao.
2) Kuimarisha Ukaguzi wa Madini.
3) Kukamilisha Upembuzi Yakinifu juu ya uingizaji wa madini ya ujenzi Zanzibar.
4) Kuongezeka kwa Ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Maliasili Zisizorejesheka.
5) Udhibiti wa Uchimbaji Holela wa Maliasili Zisizorejesheka.
6) Uhuishaji wa maeneo yaliyochimbwa mchanga.
7) Kutenga Maeneo Maalum kwa ajili ya Uchimbaji.
8) Ujenzi wa Maabara ya Jiolojia ya Madini.

**Changamoto katika Sekta ya Madini**

Changamoto zinazoikabili sekta ya madini ni kama zifuatazo:-

a) Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutekeleza miradi mbali mbali nchini ikiwemo ya barabara, bado kuna baadhi ya gari zinauza kwa wananchi kifusi kinachotolewa na Serikali bila ya malipo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambapo inapelekea kuzorota kwa ukusanyaji wa mapato ya Serikali.
b) Baadhi ya gari zinazotumika kusafirisha Maliasili Zisizorejesheka kutofuata vipimo vya upakizi vilivyowekwa pamoja na kutofunika vizuri, jambo linalohatarisha maisha ya wananchi na kupelekea ajali barabarani ikiwemo kurusha vumbi na kuharibu vyombo vengine vya usafiri na kuchafua barabara kwa kudondosha mawe, vifusi na kokoto.
c) Kuendelea kuripotiwa kwa vitendo vya uchimbaji holela wa Maliasili Zisizorejesheka kwa baadhi ya maeneo pamoja na baadhi ya viongozi wa Serikali za

maeneo husika kutuhumiwa kujihusisha na vitendo vya uchimbaji haramu wa Maliasili Zisizorejesheka.

d) Kuchelewa kupatiwa kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya jiolojia ya madini.
e) Baadhi ya Taasisi za Serikali kusafirisha Maliasili Zisizorejesheka bila ya kufuata utaratibu ikiwemo kutokuomba vibali jambo ambalo linapunguza ukusanyaji wa mapato.
f) Kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwa baadhi ya watendaji wa Idara hasa katika maeneo ya machimbo, vituo vya ukaguzi na doria.
g) Baadhi ya Taasisi za Serikali hazitoi ushirikiano wa kutosha katika kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya madini hasa katika eneo la ulinzi wa Maliasili Zisizorejesheka.
h) Baadhi ya miti katika maeneo yaliyohuishwa imeshindwa kukua kutokana na kukosa ushughulikiaji mzuri na baadhi ya wafugaji kutumia maeneo hayo kama malisho ya wanyama.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaiomba Wizara kuwasiliana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ili iwasimamia vyema wakandarasi ambao ndio wamiliki wa gari zinazotumika kusafirisha Maliasili Zisizorejesheka katika maeneo ya miradi pamoja na kuzichukulia hatua za kisheria gari zinazobainika kufanya makosa hayo.
2) Kamati inaiomba Wizara kuharakisha ununuzi wa mizani ambao utaondoa changamoto za wananchi wanaojaza mali zisizorejesheka kupita katika alama iliyowekwa kwani mizani hizo zitakuwa na uwezo wa kupima kiwango halisi cha rasilimali kilichopakiwa na mwanachi kulipia pamoja na ongezeko.
3) Kwa mara nyengine tena, Kamati inaiomba Wizara kuendelea na doria pamoja na kuimarisha kikosi cha doria kwa kuomba askari wa ziada kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ili kuweza kukabiliana kikamilifu na uchimbaji holela wa Maliasili Zisizorejesheka.

4) Wizara iendelee kuzikumbusha Taasisi za Serikali juu ya kufuata utaratibu wa uchimbaji na usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka ili kuepuka usumbufu wakati wa utekelezaji wa miradi yao.
5) Kamati inaishauri Wizara kupitia idara ya Nishati na Madini kutafuta utaratibu mzuri wa kupata usimamizi wa maeneo yanayohuishwa, ili uhuishaji huo uweze kuwa na matokeo Chanya.

### 4:4:3 Maliasili Zisizorejesheka

Maliasili Zisizorejesheka zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Zanzibar. Ujenzi wa miradi mbalimbali inayoendelea hivi sasa ikiwemo ujenzi wa hospitali za Wilaya, skuli za ghorofa, masoko na barabara umekua ukitumia mchanga, kokoto na kifusi kwa kiwango kikubwa wakati wa ujenzi.

### Uchimbaji na Usafirishaji wa Maliasili Zisizorejesheka

Kumekuwa na utaratibu wa kuwepo kwa vituo vya maegesho ya gari kwa ajili ya kusubiri wahitaji wa maliasili hizo. Vituo hivyo vimekuwa ni kitovu cha uuzaji wa Maliasili Zisizorejesheka haramu (zinazochimbwa bila ya kufata utaratibu) hususan mchanga. Kadhalika, uchafuzi wa mazingira na jamii kwa ujumla umekuwa ni changamoto katika maeneo hayo. Uchunguzi wa Kamati umegundua kuwa Zanzibar kuna maeneo ya uegeshaji wa magari kama inavyoonekana kwenye jadweli lifuatalo:

| WILAYA | ENEO/SHEHIA |
|---|---|
| Mjini | Hakuna |
| Magharibi ‘A’ | Mwera Kidarajani |
| | Mbuzini |
| Magharibi ‘B’ | Kisauni |
| | Meli Nne |
| Kati | Jumbi Sokoni |
| Kusini | Njia ya Mtende |
| Kaskazini ‘A’ | Kidoti |
| Kaskazini ‘B’ | Fujoni |

**Athari Zinazojitokeza Katika Maeneo ya Uegeshaji**

Changamoto zilizoibuliwa na Kamati katika maeneo ya uegeshaji wa gari zinazosafirisha rasilimali zisizorejesheka ni kama zifuatazo: -

a) Kuendelea kwa vitendo vya uchimbaji holela wa mchanga katika maeneo yasiyo rasmi hali ambayo inaharibu mazingira pamoja na ukosefu wa mapato ya Serikali;
b) Kuvamiwa kwa maeneo ya hifadhi ya njia kuu ya umeme itokayo Fumba kuelekea Meli Nne TAVETA;
c) Uchafuzi wa mazingira unaoweza kupelekea maradhi ya mripuko ikiwemo malaria na kipindpindu;
d) Vitendo vya utumiaji wa madawa ya kulevya ikiwemo bangi ambapo inaweza kuhatarisha ustawi wa jamii iliyopo maeneo ya karibu na sehemu ya maegesho;
e) Kupelekea wananchi wenye uhitaji wa Maliasili Zisizorejesheka kukosa rasilimali hizo kwa mujibu wa mahitaji yao kutokana na uchache wa rasilimali uliosababishwa na gari ambazo zimechukua rasilimali hizo bila ya kuwa na matumizi sahihi.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Kamati inaiomba Wizara na Serikali kwa ujumla kuwaangalia kwa jicho la huruma wananchi waliopo katika eneo la magari ya mawe Meli Nne TAVETA kutokana na athari wanazoendelea kuzipata kutokana na kuwepo kwa kituo hicho cha magari ya rasilimali zisizorejesheka katika maeneo hayo;
2) Wizara iendelee kutafuta maeneo maalum ya maegesho ya gari za kutoa huduma za usafirishaji wa Maliasili zisizorejesheka kwa wananchi wenye mahitaji madogo;
3) Wizara ifanye doria na zoezi la ukaguzi wa kushtukiza katika maeneo mbalimbali ya maegesho kwa lengo la kubaini gari zilizopakia Maliasili Zisizorejesheka bila ya kuwa na kibali.

## 4:5 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR (ZECO)

Shirika la Umeme Zanzibar linajukumu la kuwezesha uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na uuzaji wa Umeme Zanzibar.

### Hali ya Miundombinu ya Umeme Unguja na Pemba

Kamati imepokea taarifa kwamba Visiwa vya Unguja na Pemba vinapata umeme kupitia waya za baharini zenye uwezo wa Megawati 100 na Megawati 45 za mkondo wa Kilovoti 132 kwa upande wa Unguja na Megawati 20 za Mkondo wa Kilovoti 33 kwa upande wa Pemba kutoka Gridi ya Taifa ya Tanzania Bara.

Kamati imebaini kuwa kutokana na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ndani ya visiwa vya Zanzibar matumizi ya umeme yameendelea kukua na kuongezeka kwa wastani wa megawati 15 baina ya mwaka 2021 hadi mwaka 2023 ambapo mahitaji ya juu yamefikia Megawati 112.13 (Megawati 91 kwa waya wa kilovolt 100 na Megawati 21.13 kwa waya wa kilovoti 45) sawa na asilimia 77.33 kwa waya zote mbili zilizopo. Aidha, kwa upande wa Pemba mahitaji ya juu ya umeme yamefikia megawati 13.16 sawa na asilimia 65.8 ya uwezo wa waya unaotumika hadi sasa wa Megawati 20.

### Mafakikio ya ZECO Kuanzia Julai – Disemba, 2023

Shirika la Umeme limepanga kusambaza huduma ya umeme katika vijiji 35, ambapo Unguja 18 na Pemba 12. Katika utekelezaji wa kazi hiyo, Shirika limeweza kupeleka huduma ya umeme katika vijiji 22 kwa Unguja na vijiji 13 kwa Pemba sawa na asilimia 53.33 ya vijiji vilivyopangwa.

Aidha, katika kazi ya ubadilishaji wa nguzo mbovu, Shirika limefanikiwa kubadilisha jumla ya nguzo mbovu 1160 (909 Unguja na 251 Pemba). Vile vile, kazi ya ukaguzi wa transfoma, Shirika limefanikiwa kufanya ukaguzi wa jumla ya transfoma 638 (Unguja 444 na Pemba 194). Ukaguzi huo ni sawa na asilimia 77.24 ya transfoma 826 (Unguja 600 na Pemba 226) zilizopangwa kukaguliwa katika kipindi hicho. Pia, ZECO imefanikiwa kuwaunganishia huduma ya umeme jumla ya wateja wapya 17,251 (14,461 Unguja na 2,790 Pemba),

ambapo ni sawa na asilimia 90 ya wateja 19,200 (Unguja 15,600 na Pemba 3,600) waliopangwa kuunganishiwa umeme katika kipindi hicho.

**Hali ya Madeni ya Wateja wa ZECO**

Kamati imebaini kwamba katika utekelezaji wa majukumu yake, Shirika la Umeme Zanzibar limekuwa likikabiliana na changamoto mbali mbali ikiwemo ya ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wateja wake.

Hadi Disemba 2023, Shirika linawadai wateja wake Unguja na Pemba jumla ya **TZS. Bilioni 65,091,321,485.93,** ambapo mchanganuo wake kama ifuatavyo; -

***Jadweli 4: Madeni ya wateja wa  Umeme hadi Disemba 2023.***

| Maelezo | Unguja | Pemba | Jumla |
|---|---|---|---|
| SMZ-ZAWA | 32,571,789,190.25 | 24,596,845,014.43 | **57,168,634,204.68** |
| SMZ - NYENGINEZO | 4,387,939,222.09 | 334,037,043.68 | **4,721,976,265.77** |
| SMT | 1,798,694,904.16 | 525,326,374.40 | **2,324,021,278.56** |
| WATEJA BINAFSI | 847,599,051.26 | 29,090,685.66 | **876,689,736.92** |
| **JUMLA KUU** | **39,606,022,367.76** | **25,485,299,118.17** | **65,091,321,485.93** |

*Chanzo: ZECO, 2023*

**Changamoto za ZECO**

a) Utaratibu usioepukika wa matumizi ya umeme kabla ya malipo.
b) Uwepo wa malimbikizo ya madeni kwa wateja wa Shirika la Umeme unatokana na baadhi ya wateja kushindwa kulipa ankara zao za matumizi ya umeme kwa ukamilifu na wakati.
c) Shirika kushindwa kupata fedha zake kutoka kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), licha ya juhudi za mazungumzo yanayoendelea chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar.
d) Uharibifu wa Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme kama vile uchimbaji wa mchanga kwenye njia kuu za umeme na wizi wa Nyaya za shaba.

e) Kamati imebaini kuwepo kwa ubadilishaji wa nguzo mbovu unaofanyika mara kwa mara, jambo linalotia wasiwasi juu ya uimara wa nguzo hizo.

f) Baadhi ya wateja wasiokua waaminifu kutumia umeme kinyume na utaratibu, hali inayopelekea Shirika kukosa mapato yake stahiki.

g) Uvamizi katika njia kuu za usambazaji wa umeme kupitia shughuli za kijamii ikiwemo ujenzi, uchomaji moto, ufanyaji wa biashara na ufugaji.

**h)** Ukosefu wa ukarimu wakati wa kutoa huduma (*Customer care)* ambapo baadhi ya watendaji hutoa majibu yasiyoridhisha kwa wateja na kupelekea wananchi kukosa imani wakati wanapohitaji huduma.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

1) Shirika na Wizara kwa ujumla ifanye utafiti kwa lengo la kubaini utaratibu mzuri wa malipo ya matumizi ya umeme ukilinganisha na uliopo hivi sasa ikiwa ni njia moja wapo ya kudhibiti hali ya madeni iliopo.
2) Shirika na Wizara kwa ujumla iendelee kufanya mazungumzo na Taasisi za Serikali (SMZ na SMT), ili kusawazisha madeni yaliyopo pamoja na kufanya malipo ipasavyo kwa mujibu wa matumizi yao ya umeme ya kila mwezi kwa taasisi hizo.
3) Shirika liongeze bidii ya utoaji wa elimu kwa umma juu ya madhara na athari zinazotokana na uvamizi, wizi na uharibifu wa miundombini ya umeme.
4) Kamati inashauri na kusisitiza nguzo zinazobadilishwa ziwe zenye viwango na uimara zitakazopelekea kudumu kwa muda mrefu kulingana na maeneo yaliyopo kama vile sehemu za mabondeni pamoja na kufikiria kuanza matumizi ya nguzo zilizotengenezwa kwa zege au chuma ili kupunguza ubadilishaji holela wa nguzo hizo.
5) Kamati inaishauri ZECO kufanya Utafiti wa Uondoshaji wa Nguzo za Kuninginiza waya Juu na badala yake kuangalia uwezekano wa kutisha umeme Chini ya Ardhi kwa kutumia waya Maalum (Amal Cable).

6) Kamati inapendekeza elimu ya utoaji huduma bora kwa wateja iwe inatolewa mara kwa mara hasa kwa watendaji wanaohusika na Wizara hii ya Maji, Nishati na Madini ili waweze kushirikiana kwa pamoja kutoa huduma nzuri na zenye tija kwa wananchi.

## 4:6 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI (ZURA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar – ZURA ilianzishwa kwa Sheria Namba 7 ya mwaka 2013, majukumu yake ni kudhibiti huduma za maji na nishati ya mafuta, gesi na umeme, ili kuhakikisha huduma hizo zinapatikana kwa kiwango bora.

### Wigo wa Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati

Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba kwa ujumla udhibiti wa ZURA kwenye huduma unazingatia utoaji wa leseni, udhibiti wa tozo kwa kushauriana na Waziri husika, kukuza ushindani mzuri wa ufanisi kwenye Uchumi, kudhibiti ubora wa viwango pamoja na kusimamia mikataba yote inayohusiana na uuzaji wa nishati na maji.

### Udhibiti wa Huduma za Maji

Kwa kipindi hiki, ukaguzi katika vyanzo vya Uzalishaji na Miundombinu ya Maji ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za maji pamoja na usalama wa vyanzo vinavotumika kuzalisha maji, ZURA ilifanya ukaguzi katika wilaya ya Magharibi 'A', Kaskazini "A" na "B". Jumla ya visima sitini na nane (68) vinavyotumika kuzalisha maji pamoja na miundombinu yake ilikaguliwa, kati ya hivyo visima hamsini na tano (55) vinafanya kazi na kumi na tatu (13) havifanyi kazi.

### Changamoto zilizobainika katika ukaguzi wa miundombinu na mazingira ya vituo vya uzalishaji maji Unguja ni: -

a) Visima kukosa uzio ambao unatoa uhifadhi mzuri wa vyanzo hivyo.

b) Kuwepo kwa mazingira yasiyoridhisha katika baadhi ya "Pump House" na miundombinu ya visima zikiwemo "Well Head".

c) Kukosekana vifaa vya dharura wakati wa hatari katika vituo vyote.

d) Kukosekana pampu ya dharura (standby pump).

e) Kukosekana kwa taarifa za kiwango (Ujazo) cha maji yanayozalishwa na kusambazwa.

**Changamoto zilizobainika katika ukaguzi wa miundombinu na mazingira ya vituo vya uzalishaji maji Pemba ni: -**

Kamati pia ilipokea taarifa ya ZURA kuhusiana na Ukaguzi wa visima kwa upande wa Pemba, ambapo visiwa 79 kati ya 131 vimekaguliwa ubora wake wa maji katika Wilaya ya Wete, Mkoani na Micheweni na kubainika yafuatayo: -

a) Visima 30 havina uzio kabisa.

b) Visima vitatu (3) uzio wake ni mbovu.

c) Visima 6 vimekosa mfuniko wa juu.

d) Visima vingi vinavujisha na kuachwa muda mrefu bila ya kufanyiwa usafi.

**Udhibiti wa Maji Taka (Maji Machafu)**

Katika hatua nyengine, Kamati imebaini kwamba ZURA imeanza hatua za kudhibiti maji taka (Maji Machafu), ambapo imeandaa hadidu rejea (*Terms of Reference-TOR*) kwa ajili ya kumtafuta mshauri elekezi kwa ajili ya *Development of Country Sanitation Road Map*. Hata hivyo, mchakato huo bado upo katika hatua ya manunuzi ili kupatikana mshauri elekezi atakaekidhi vigezo kwa ajili ya uandaaji wa *Sanitation Road Map*.

**Udhibiti wa Huduma za Umeme**

Kwa upande wa udhibiti wa huduma za Umeme, Kamati imejuilishwa kwamba Mamlaka imefanya ukaguzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Wilaya ya Kaskazini "A" na "B" Magharibi B na Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuchagua maeneo ya njia za kusambaza umeme kwa lengo la kutambua hali halisi ya huduma inayotolewa kwa wananchi, ambapo jumla ya vituo hamsini na nane (58) vilikaguliwa katika njia ya

kusambaza umeme (Distribution Feeder). Kati ya hivyo, vituo 31 ni vya Kaskazini Mpya na Kaskazini Kongwe.  kwa upande wa Pemba, Mamlaka, imefanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme kwa kukagua transfoma zilizopo katika laini ya CBMP Kaskazini, transfoma zilizopo katika kisiwa cha Fundo na kituo cha kuzalishia umeme utokanao na Nishati Mbadala ya jua katika kisiwa cha Kokota.

**Kasoro Zilizobainika Kupitia Ukaguzi wa ZURA Katika Maeneo ya ZECO Yaliyoainishwa Hapo Juu ni Kama Zifuatazo: -**

a) Transforma katika sehemu za kupokelea umeme mkubwa (High Voltage) zimeungwa moja kwa moja kwa kutumia waya (fuse element), baadhi ya maeneo hayo ni Mbweni Karume, Barabara ya Buyu, Dimani Bondeni (ZAWA) na Bweleo kwa Mkorea, maeneo mengine ni Nungwi njia ya Mnarani, Mchekeni, Kiwengwa Kumba Urembo na Matemwe Mbuyutende mwisho.

b) Transfoma kukosa alama za tahadhari pamoja na kuzungukwa na majani.

c) Katika kituo cha kusambaza umeme cha Nungwi njia ya Mnarani nguzo zilizoekewa transfoma ni mbovu.

d) Katika kituo cha kusambaza umeme cha Tomondo Changu, Fumba Kijijini pamoja na Nyamanzi njia ya Fumba nguzo zilizoekewa transfoma ni mbovu, zinahitaji kubadilishwa kwa usalama wa transfoma na watumiaji.

e) Katika vituo vya kusambaza umeme vya Chukwani Kituo cha Daladala, Dimani Bondeni (ZAWA), Bwefumu Skuli n.k ambapo miundombinu yake ya ufungaji wa waya (Transformer Dressing) haziko katika hali nzuri.

f) Aidha, katika baadhi ya vituo vya kusambazia umeme waya za usalama wa transfoma zimekatwa.

***g)*** Katika baadhi ya vituo Transfoma zilizopo zinatumia njia moja ya kusambaza umeme badala ya kutumia njia tatu na kusababisha umeme mdogo kwa watumiaji.

**Udhibiti wa Huduma za Mafuta**

Mamlaka imefanya ukaguzi wa Bohari tano (5), Nne (4) kwa upande wa Unguja na moja (1) kwa Pemba, na ukaguzi wa vituo vya mafuta ambapo jumla ya vituo mia na tano (105) vilikaguliwa, vituo themanini na sita (86) kwa Unguja na kumi na tisa (19) kwa Pemba. Hadi kufikia Disemba, 2023 jumla ya vituo viwili (2) havikuweza kutoa huduma. Kati ya vituo hivyo, kituo kimoja kimefungiwa kwa kukiuka masharti ya kiudhibiti ambacho ni kituo cha Coral Reef (Nungwi), na kituo cha pili ni Kiwengwa Petrol Station ambacho bado kipo katika matengenezo.

**Malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati.**

Mamlaka imefanya Mikutano miwili (2) kwa ajili ya kutatua malalamiko kwa njia ya usuluhishi na pia ilipokea na kuchunguza Malalamiko kupitia maeneo makuu ya Umeme, Mafuta Gesi na Ulipaji wa fidia kwa wananchi wa Mwangapwani, kama inavyoonekana katika Jedweli lifuatalo: -

***Jadweli 5 Malalamiko yaliyopokelewa ZURA na kushughulikiwa.***

| Na | Aina | Maelezo | Hatua ilofikia |
|---|---|---|---|
| 1. | Umeme | Umeme mdogo Jambiani | Lipo katika hatua za kusubiri majibu kutoka ZECO. |
| | | Umeme mdogo Bwejuu | Lipo katika hatua ya kusubiri majibu kutoka ZECO |
| | | Umeme mdogo Dole | Limeshatatuliwa |
| 2. | Mafuta | Kuchanganyika Maji na Mafuta | Limeshatatuliwa |
| 3. | Fidia Mangapwani | Fidia Mangapwani | Ipo katika uhakiki Mkoa wa Kaskazini Unguja |
| 4. | GESI | Ubadilishwaji wa mitungi ya Gesi bila ya ridhaa ya Kampuni | Lipo katika hatua ya uchunguzi |

***Chanzo: ZURA 2023***

**MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI**

1) Kamati inaishauri ZURA kuchukua hatua kwa kuitaka ZECO na ZAWA kufanya marekebisho ya kasoro zilizojitokeza pamoja na kuzingatia taratibu za kiusalama na ubora wa huduma za umeme na maji yanayosambazwa kwa wananchi.

2) Kamati inaiomba ZURA kuendelea kutoa miongozo na maelekezo ya kitaalamu ikiwa ni pamoja na kushirikiana na wataalamu wa ZECO na ZAWA katika kurekebisha dosari zilizobainika.

## 4:7 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Kamati ilipokea taarifa ya wizara kuhusiana na utekelezaji wa Miradi mbali mbali inayotekelezwa chini ya usimamizi wa wizara hii. Baadhi ya miradi hiyo taarifa zake ni kama zinavyoelezwa hapo chini; -

### 4:7:1 Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar

Mradi huu unagharimu USD milioni 92.18 sawa na TZS. bilioni 211.83 ambazo ni mkopo kutoka **Benki ya Exim** ya India. Mradi huu unahusisha uchimbaji wa visima, ujenzi wa matangi, ulazaji wa mabomba na ujenzi wa jengo la Afisi kuu ya ZAWA. Hadi kufikia Disemba, 2023 mradi huu umefanikiwa kutekeleza kazi zifuatazo: -

**a) Uchimbaji wa visima:** Kazi ya uchimbaji wa visima 64 imekamilika sawa na 100% ya makadirio katika maeneo ya Dole (8), Kidutani (14), Dimani (5), Mfenesini (10) Maungani (9), Mkorogo (8) na Masingini (10).

**b) Ujenzi wa matangi 15 ya kuhifadhia maji:** Ujenzi wa matangi katika maeneo yote umefikia wastani wa asilimia 96 ambapo kwa LOT 1 (Mfenesini na Dole) umefikia wastani wa asilimia 95 kwa upande wa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) umefikia wastani wa asilimia 97, na LOT 3 (Kidutani na Masingini) ujenzi wa matangi umefikia wastani wa asilimia 99.

**c) Ulazaji wa mabomba:** Kazi ya ulazaji wa mabomba imefikia wastani wa kilomita 450.8 kati ya kilomita 466.9 sawa na asilimia 97.1 ya makadirio ambapo kwa LOT 1

(Mfenesini na Dole) zimefikia kilomita 176.57, Kwa LOT 2 (Mkorogo, Maungani, na Dimani) kilomita 151.34 na LOT 3 (Kidutani na Masingini) kilomita 122.9.

**d) Ujenzi wa Jengo la Afisi:** Ujenzi wa jengo la Afisi za makao makuu ya Mamlaka ya Maji (MAJI HOUSE) umekamilika kwa wastani wa asilimia 92%.

### 4:7:2 Mradi wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji Zanzibar kupitia fedha za ahueni ya Uchumi na Ustawi wa Jamii UVIKO - 19 kwa Upande wa ZAWA

Kamati ilijuilishwa kwamba ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Zanzibar Serikali imetenga jumla ya **TZS. Bilioni 34,200,000,000** kupitia fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya kutekeleza programu ya kuhuisha ustawi wa uchumi na kijamii kutokana na athari za UVIKO-19 kutoka shirika la fedha duniani IMF kwa kazi za uchimbaji wa visima (38), ukarabati wa visima (36), ununuzi na ufungaji wa pampu 51, uboreshaji na ubadilishaji wa mtandao chakavu kwa masafa ya kilomita 319, ujenzi wa Matangi (10) na ukarabati wa Matangi (3) na ujenzi wa vibanda 51 kwa Unguja na Pemba. Hadi kufikia Disemba, 2023 kazi zifuatazo zimefanyika: -

a) **Uchimbaji wa visima:** Wizara imefanikiwa kuchimba visima 38, visima 11 - Unguja ambavyo tayari vimekamilika na visima 27 vimechimbwa katika maeneo mbali mbali ya Pemba, kazi ya uchimbaji wa visima imekamilika kwa asilimia 100%.

b) **Ujenzi wa matangi:** Kazi ya Ujenzi wa Matangi 10 ya kuhifadhia maji imefikia wastani wa asilimia 99.96% kwa Unguja na Pemba. Aidha, ujenzi wa matangi ya Pujini na Shumbamjini umekamilika, hatua inayoendelea kwa sasa ni ulazaji wa mabomba kwa ajili ya kujaza maji katika matangi hayo.

c) **Ujenzi wa Vibanda:** Kazi ya ujenzi wa vibanda 51 vya kuhifadhia mitambo ya kuendeshea pampu imekamilika kwa wastani wa asilimia 98 kwa upande wa Unguja na Pemba.

d) **Uchimbaji wa Misingi na Ulazaji wa Mabomba:** Kazi ya uchimbaji wa misingi na ulazaji wa mabomba kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2023 imefanyika ambapo jumla ya kilomita 91.896 zimelazwa, Unguja (49.008) na Pemba (42.888) na

inaendelea katika maeneo mengine ya Unguja na Pemba. Hadi sasa kazi ya ufukiaji wa mabomba imefikia kilomita 216.497 kati ya kilomita 319.

### 4:7:3 Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Zanzibar (JICA)

Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya ZAWA na Japanese ODA Loans kwa gharama za Dola za Kimarekani Milioni 100 sawa na Yeni 10,864 Milioni na unatarajiwa kuchukua kipindi cha miezi 36. Kazi ya mradi ni uboreshaji wa miundombinu ya usambazaji maji mjini Zanzibar. Hatua iliyofikiwa ni makubaliano ya kuanza mradi kwa kazi ya usanifu wa mradi huo, kazi inayotarajiwa kufanywa na Mshauri Elekezi (Nippon Koei) na tayari Mshauri Elekezi anaendelea na kazi.

### 4:7:4 Utambuzi na Usajili wa visima binafsi

Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Maji Zanzibar na Shirika la umoja wa mataifa la kuhudumia watoto duniani (UNICEF) kwa gharama za Tzs 247,000,000, kazi ya Mradi huu ni utambuzi na usajili wa visima binafsi Zanzibar imekamilisha zoezi hilo kwa utambuzi wa visima 22,626, visima 18,828 vimetambuliwa kwa Unguja na 3,798 kwa upande Pemba. Hatua inayofuata ni kuweka nambari za utambuzi (Code) kwenye visima vilivyotambuliwa na kufanyiwa usajili pamoja na kukagua ubora wa maji.

### 4:7:5 Mradi wa Uhuishaji na Usambazaji Maji (NEC)

Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya SMZ/ZAWA na Kampuni ya National Energy Centre (NEC) ya Oman kwa gharama za dola za Kimarekani Milioni 26. Kazi za mradi ni uimarishaji wa huduma ya maji endelevu katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Hadi tunatayarisha ripoti hii hatua iliyofikiwa ni kukamilisha masuala ya fedha ambayo yapo Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili mradi/ujenzi uanze kutekelezwa.

### 4:7:6 Mradi Wa Mabadiliko ya Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Huduma ya Umeme Zanzibar (ZESTA)

Mradi huu umeanza mwaka 2021 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027. Mradi huu una lengo la kuimarisha Sekta ya umeme nchini kwa kukarabati miundombinu, kujenga line kubwa ya usafirishaji umeme (132kV) kutoka Welezo hadi Ubago na kuelekea kusini hadi

Makunduchi na kaskazini hadi Matemwe kwa Unguja. Aidha, mradi huu utajenga mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua kwa kiwango cha megawati (18MW) ambapo mtambo huo pia utajumuisha uhifadhi wa umeme huo kwa kiwango cha megawati hour (40MWh) Mradi huu unakusudiwa kufanya shughuli zifuatazo; -

a) Ujenzi wa njia kuu ya kusafirishia umeme Mkondo wa 132Kv.

b) Kuandaa ripoti ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakao athirika na ujenzi wa njia kuu ya kusafirishia umeme yenye mkondo wa 132kV.

c) Utekelezaji wa kipengele cha Jinsia.

d) Kuijengea uwezo Sekta ya Nishati.

**MAONI, MAPENDEKEZO NA USHAURI WA KAMATI**

1) Kamati inashauri Wizara kwenye miradi mikubwa iliyokamilika kwa asilimia kubwa iendane na lengo lililokusudiwa la upatikanaji wahuduma ya maji safi na salama kwa wananchi.

2) Kamati inapendekeza kwa Wizara kuwa miradi inayofanywa sasa na Serikali ni mikubwa na inatumia gharama kubwa hivyo, Serikali waisimamie vizuri miradi hiyo ili kuwa endelevu (sustainability).

## SEHEMU YA TATU

### 5:0 HITIMISHO

Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Manaibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu pamoja na viongozi na watendaji wote kwa ujumla wa Wizara zote tatu (3) zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamin wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Aidha, Kamati inatambua, kuthamini na kushukuru kwa ushirikiano mkubwa iliyoupata kutoka Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuweza kufanikisha ziara ya kuijengea Uwezo Kamati na Kujifunza huko Tanzania Bara katika Taasisi mbali mbali ikiwemo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wakala wa Barabara (TANROADS), Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICOT), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF), Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) pamoja na TEMESA.

Sambamba na hilo, Kamati tunaishukuru Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi nayo kwa kutupeleka katika ziara ya kimafunzo katika maeneo yaliyotengwa, kufanyiwa utambuzi na kupimwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makaazi katika maeneo ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma pamoja na Shirika la Nyumba la Taifa ili kuongeza uelewa juu ya masuala ya Maendeleo ya Makaazi.

Aidha, ziara kama hiyo iliandaliwa kwa Kamati na Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Shirika la Umeme ZECO kwa lengo la kujifunza Masuala ya Uzalishaji wa Umeme wa Gesi Kinyerezi Dar es Salaam pamoja na Vituo vya Kusafirishia Umeme vya Tegeta na Ras Kiromoni. Vilevile, Kamati iliweza kujifunza masuala ya Uzalishaji wa Umeme wa Maji huko Hale (Mto Pangani) Mkoani Tanga. Ziara zote hizo zilikuwa na manufaa makubwa ya

kutuongeza uelewa na hatimae tukaweza kuishauri vyema Serikali kupitia Sekta hizo. Kamati inashauri ziara kama hizo za kimafunzo ziendelezwe kadri hali itakavyoruhusu ili kuzidi kuwajengea uwezo waheshimiwa wajumbe.

Mwisho, Kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Afisa Mdhamini Afisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba ndugu Abdulghani Abdullah Said, Wakurugenzi wote wa Baraza,  Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamad Haji pamoja na sekretarieti yote ya Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati yetu kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha Ripoti yake kwa mwaka 2023/2024. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.